**31 AGOSTI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

### Kikao cha Tatu – Tarehe 31 Agosti, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Maelezo ya Waziri wa Viwanda na Biashara juu ya Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya Mwaka 2012 *(SADC Protocol on Trade in Services, 2012)*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Kilimo na Mifugo kwa niaba yake Mheshimiwa Khadija, Mjumbe wa Kamati.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo juu ya Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya mwaka 2012 *(SADC Protocol on Trade in Services, 2012)*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tunashukuru sana

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA- KATIBU MEZANI**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali tunaanza na Ofisi ya Rais, Utumushi na Utawala Bora. Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 41

**Marekebisho ya Sheria za Utumishi zilizopitwa na wakati**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itarekebisha Sheria za Utumishi zilizopitwa na wakati hasa kipindi hiki cha teknolojia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kujibu swali la Mheshimiwa Janejelly James Ntate, naomba uniruhusu nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuendelea kudumu katika Wizara hii ya Utumishi na Utawala Bora. Sasa naomba kujibi swali la Janejelly James Ntate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janejelly James Ntate, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa maendeleo makubwa ya kiteknolojia ambayo yamekuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha utendaji kazi katika utumishi wa Umma. Ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia, Serikali imeendelea kufanya mapitio ya Mfumo wa Kisheria unaosimamia Utumishi wa Umma ambapo mwaka 2019 Serikali ilitunga Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao Namba10 ya Mwaka 2019 ili kuweka mazingira wezeshi ya matumizi ya teknolojia katika utendaji kazi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitishwa kwa Sheria hiyo kumeisaidia Serikali kuboresha utendaji kazi wake kupitia matumizi ya teknolojia. Pamoja na mambo mengine Sheria hiyo imewezesha kusanifiwa na kujengwa kwa jumla ya mifumo zaidi ya 860 ya TEHAMA Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na hatua za kupitia na kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali zinazosimamia Utumishi wa Umma na Kanuni zake ili kuhakikisha kwamba zinaendana na mabadiliko ya teknolojia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janejelly, swali la nyongeza.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali na niwapongeze kwa juhudi mnazofanya za TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona sasa hivi kuna utaratibu wa viongozi wa aina moja au Maofisa wa aina moja kufungua *group* na kutumiana *document* za kiserikali ndani ya *group*. Je, hiyo sheria mliyoitunga imejua na hiyo kwamba imo huo au haimo?

Je, kama haimo na hairuhusiwi mnafanya nini ili sheria i-*accommodate* ili kuwaepusha wanaotumia huo mtandao wasije kupatwa na matatizo ya kuhukumiwa na hiyo Sheria ya kuwa na Nyaraka za Serikali kwa sehemu zisizo husika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inayosimamia nyaraka za Serikali inaelekeza wazi kwamba mawasiliano ya Serikalini yafanyike kwa njia ya barua lakini haielekezi vinginevyo. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako kwamba haitokuwa sawa na ni marufuku ya Serikali kuwasilisha au kutumiana *document* za Kiserikali kupitia njia ya *WhatsApp* na njia nyingine zisizo rasmi isipokuwa kwa yale maelekezo ambayo yatakuwa yametolewa vinginevyo katika mamlaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa swali la nyongeza.

Kutokana na jibu la msingi ambalo Mheshimiwa Waziri umelitoa hauoni kwamba bado tutakuwa nyuma ya teknolojia kwa sababu mwisho wa siku tunahitaji kuweka mifumo ambayo itazilinda hizo *document* lakini ziende kwa haraka kwa sababu teknolojia inasaidia kufanya kazi kwa haraka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakagenda, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati najibu swali la msingi nimeeleza mpaka sasa baada ya kupitishwa kwa Sheria Namba Kumi ya mwaka 2019 Serikali imekwisha tengeneza au kujenga mifumo ya TEHAMA zaidi ya 860 kwa ajili ya kusimamia utendaji wa Serikali. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mwakagenda kwamba Serikali bado inaendelea kuitengeneza mifumo mbalimbali itakayosimamia ambayo italeta Serikali yote katika adabu ya kiutendaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii Wizara ndiyo inahusika na masuala ya *TASAF* watu wangu wa Jimbo la Bunda kumekuwa na matatizo makubwa sana ya malipo ya *TASAF* karibu nchi nzima, naomba Waziri atamke kwamba kuna nini kinachoendelea katika *TASAF?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Getere, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Getere najua swali lake linatokana na ukweli kwamba yako baadhi ya matatizo au changamoto zilizojitokeza katika utendaji ndani ya Taasisi yetu inayosimamia Mfuko wa Kunusuru Kaya Maskini yaani *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba yako maamuzi na maelekezo makubwa yaliyokwishafanyika ambayo sasa yale mapungufu yote yaliyojitokeza au mapungufu kwa asilimia kubwa yaliyojitokeza ndani ya *TASAF* tunaweka sawa. Nataka nimhakikishie kwamba yeye na Wabunge wote humu ndani wasiwe na wasiwasi Serikali iko kazini na kazi ya kurekebisha zile kasoro zote zinaendelea kufanyika, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, Sheria ya Utumishi inaelekeza pia likizo ni haki ya mtumishi lakini likizo ile inatakiwa iambatane na stahiki zake za usafiri au nauli kwa mtumishi, lakini mpaka sasa kuna changamoto ya Walimu kupewa likizo lakini kutokupewa nauli ya kwenda makwao. Je, nini kauli ya Serikali kuhusiana na jambo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali imekuwa inapokea malalamiko ya watumishi juu ya baadhi ya madai au malimbikizo ya madai kama ambavyo ameeleza Mheshimiwa Mbunge lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali imeendelea kufanya hatua za malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe taarifa mbele ya Bunge lako kwamba hadi sasa tunapozungumza Serikali imekwishalipa zaidi ya wafanyakazi 126,924 ambao kwa gharama ya kifedha ni sawasawa na bilioni 216 kwenda kulipa madeni yote ambayo yanaendelea, ninachoweza kusema katika Bunge lako wale wafanyakazi wote ambao wana madeni ya malimbikizo wawasiliane na Ofisi zetu kupitia Wakurugenzi wa Halmashauri pia kupitia Ofisi ya Rais ili madeni yao yote au madai yao yote ya malimbikizo tuweze kuyaangalia mara mara moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira sasa namuita Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Mwanga, aulize swali lake.

Na. 42

**Kuondoa magugu maji katika Ziwa Jipe**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi wa kuondoa magugu maji katika Ziwa Jipe?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Mwanga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi imeona changamoto ya uharibifu wa mazingira unaotokana na kuenea kwa magugu maji katika Ziwa Jipe. Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira tayari imefanya tathimini ya uharibifu uliopo na kuandaa andiko la mradi wa hifadhi ya ardhi, na vyanzo vya maji wenye thamani ya takribani dola za Marekani milioni sita kwa ajili ya kuondoa magugu maji katika Ziwa Jipe ambapo hadi sasa jitihada za kutafuta fedha kutoka kwa wafadhili mbalimbali zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia ya Serikali kuhakikisha inarejesha ikolojia ya Ziwa Jipe ili kuleta manufaa kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo pamoja na uhifadhi wa mazingira. Serikali inamhakikishia Mbunge kwamba mara fedha zitakapopatikana itatekeleza mradi huu mara moja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Tadayo, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninapenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hilo la magugu maji katika Ziwa Jipe limedumu zaidi ya miaka 20 sasa, na imekuwa ni ahadi ya Serikali kila wakati ya kuondoa magugu maji hayo. Pamoja na shukrani kwa Mheshimiwa Rais kupitia kwa Mheshimiwa Waziri alimtuma Naibu Waziri akaja kuwapa ahadi hiyo wananchi, lakini Serikali haioni sasa kwamba umefika wakati kwa vile tatizo hili limekuwa kwa muda mrefu sana, ziko mashine hizi *aquatic wild harvesters* nyingi sana China na kila mahali ambazo thamani yake haizidi hata dola laki tano, ambazo zinaweza zikafanya kazi hii kwa namna endelevu kidogo kidogo ili kuzuia kuendelea kwa uharibifu wa mazingira na pia kuwawezesha wananchi wa Mwanga kuendelea kufaidi matunda ya lile Ziwa wakati Serikali inaendelea na mpango mkubwa huo wa mabilioni ya fedha ambao tunausubiri kwa hamu, ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la kaka yangu Mheshimiwa Joseph Tadayo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kushukuru sana Mheshimiwa Mbunge amekuwa akielezea hoja hii mara nyingi sana na ndiyo maana takribani wiki nne zilizopita nilimtuma Naibu wangu, Mheshimiwa Chilo alienda kule kwa ajili ya kuangalia uhalisia ulivyo. Kama nilivyosema ni kwamba tunaendelea na mchakato huu na andiko letu hili ni kwa ajili ya Ziwa Jipe na hali kadhalika Ziwa Chala lakini maoni ya Mheshimiwa Mbunge naomba niseme kwamba Ofisi yetu imeyachukuwa, lengo letu ni kwamba kuhakikisha tunatumia mbinu zote zinazowezekana, hili itaangalia fursa zote zinazopatikana hata tukipata mradi kidogo wa muda mfupi, nini kifanyike lakini jambo kubwa la pale litaendelea kufanyika katika mradi huu lakini lile wazo la kwanza lakini wazo lako tunalichukua kwa ajili ya kulifanyia kazi Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Vedastus Mathayo, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Victoria mwaka jana lilichafuka sana na likasababisha Samaki wengi wakafa hasa wale watu waliokuwa wametengeneza Vizimba wakapata hasara kubwa, Serikali ilipotuma wataalam waliweza kusema kwamba ni kwa sababu ya vinyesi vya mifugo kwa maana ya ng'ombe ndiyo vimesababisha hali hiyo imetokea, yale majibu hakuna yeyote aliyekubaliana nayo.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba hali hiyo haijitokezi tena ili wananchi wanaoishi Kanda ya Ziwa wasiendelee kupata hasara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mathayo, Mbunge wa Musoma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulipata changamoto sana katika Ziwa Victoria, changamoto hii ilisababishwa na suala zima la mkondo wa Mto Mara ulikuwa unashuka kule, hili kama tulivyosema ni kwamba lengo letu ni kwamba hatuhitaji wananchi waweze kupata hasara na katika hili ndiyo maana msisitizo wetu mkubwa ulikuwa ni jinsi gani wananchi kupewa elimu ya utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneno mbalimbali tulivyoona miongoni mwa changamoto kubwa inayotokea ni uhalibifu wa mazingira. Leo hii hatuzungumzii Ziwa Victoria peke yake hata Ziwa Babati hivi karibuni, unaona kwamba ongezeko la magugu maji. Ndiyo maana Ofisi ya Makamu Wa Rais, Muungano na Mazingira ilichokifanya ni nini hivi sasa? Ilichokifanya sasa hivi ni

kuandika maandiko mengi kwa pamoja na siyo linalozungumzia suala la Ziwa Jipe peke yake lakini sasa hivi tuna suala zima la Ziwa Babati, na eneo lote la Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu letu ni kuona jinsi gani tutafanya tupate mbinu mbadala ya kuhakikisha maeneo haya yote tunayatunza kwa lengo la kuwasaidia wananchi na uchumi wao. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum namuita Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 43

**Mila potofu kuwekeza mke tumboni mwa mama**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufuatilia mila potofu za kuwekeza mke akiwa tumboni mwa mama hasa Manyara na Arusha?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi kuhusu mpango gani Serikali tunao kufuatilia mila potofu za kuwekeza mke akiwa tumboni mwa mama hasa mikoa ya Manyara na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa kuna mila zenye faida ambazo zinapaswa kuendelezwa na mila zenye kuleta madhara ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziita "Mila potofu" ikiwemo mila ya kuwekeza mke akiwa tumboni mwa

mama. Mila hii ina madhara kwa kuwa inachochea ukatili wa kihisia, ndoa za utotoni na ina mnyima mhusika haki yake ya msingi ya kumchagua mwenza wa kuishi naye umri utakapofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutokomeza mila za aina hiyo, Serikali imeandaa utaratibu wa kufanya majadiliano kuhusu masuala ya kimila na majadiliano haya yanahitaji umakini mkubwa katika kuyajadili. Hivyo basi, Wizara imeandaa mwongozo wa Taifa wa uendeshaji majadiliano kuhusiana na mila na desturi zenye madhara kwa jamii wa mwaka 2022. Majadiliano hayo yanakuwa ni jumuishi yanayohusisha viongozi wa mila, viongozi wa dini, wazee maarufu na wataalam waliopo katika ngazi ya jamii ili kuja na ujumbe mahsusi wenye lengo la kutokomeza mila zenye madhara ikiwa ni pamoja na kuwekeza mke akiwa tumboni mwa mama yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito kwa Wataalam wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii waliopo ngazi za Jamii kuandaa majukwaa ya kuongoza majadiliano haya kuhusu mila hiyo yenye madhara na kuja na ujumbe mahsusi utakaotumika kutoa elimu ikiwa ni kwenye nyumba za ibada pia na kwenye redio mbalimbali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa kuozesha mtoto bila ridhaa yake ni unyanyasaji wa kijinsia; je, ni lini mwangozo huo utamalizika?

Swali la pili, je, kwa nini jambo hili lisiingizwe kwenye sheria? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo huu umeshakamilika na kinachofuata ni kuzindua. Kwa swali lake zuri la leo tutaenda kuzindulia Manyara hukohuko au Arusha na tutamualika na yeye awepo ili awe Balozi kabisa wa kubeba ujumbe huu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali pili kuhusu masuala ya sheria, ni kweli naona umuhimu huo, kwa sababu bado tunaendelea na mchakato wa maboresho ya Sheria ya Mtoto nimelipokea tutaliwasilisha kwenye Kamati waone itifaki ya kisheria kwa sasa kama inaweza kuingizwa au kunahitaji tafiti zaidi kisha tutawasilisha taarifa. Ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mkakati gani wa kubaini mila zote nzuri ili kurithisha vijana wetu wa sasa waachane na mambo ya kigeni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Toufiq, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa nchini Tanzania tunazo mila nyingi sana nzuri ambazo kwa wakati wa sasa zingetusaidia kupambana na mabadiliko ya mmomonyoko wa maadili katika dunia nzima jinsi ambavyo inakumbwa. Hivyo basi, nimepokea hoja hii, tutakwenda kuunda kikosi kazi tukishirikiana na Wizara ya Utamaduni, Michezo na Sanaa pamoja na Wizara nyingine zote tuweze kuja na *list* ya hizo mila nzuri, kwa pamoja tuweze kuweka mkakati wa kuzielimisha, kuzithibitisha na kuziweka

kwenye kumbukumbu sahihi za mila zetu ambazo tutakuwa tunazifanyia kazi Nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hivi karibuni kumeibuka utamaduni mzuri na mila nzuri sana ya kumtetea, kumlinda na kumjengea uwezo mtoto wa kike, lakini tunao utamaduni wetu ambao mtoto wa kiume ni baba au kiongozi wa familia: Je, Serikali ina mpango gani wa kumuimarisha na kumjengea uwezo mtoto wa kiume ili awe kiongozi mzuri wa familia? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha, Mbunge, swali zuri kabisa, tuna utamaduni gani wa kumjengea uwezo mtoto wa kiume? Ni kweli kabisa tunatambua sasa hivi pia mtoto wa kiume tofauti na awali anakumbwa na changamoto nyingi sana zitokanazo na mmomonyoko wa maadili, anakosa malezi na makuzi bora, kiasi kwamba sasa hata akija kuwa baba atashindwa kuwa baba mzuri wa kupambana na changamoto za familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, Serikali inatekeleza mpango wa malezi na makuzi ya watoto kwenye umri wa awali ambapo hii inaenda sambamba na ujenzi wa vituo vya kulea watoto hawa kwenye ngazi ya jamii, na kule tunakuwa na watoto wa kiume na wa kike. Tuna mpango wa pili wa kuwawezesha na kuwaendeleza vijana balehe, kuanzia miaka 10 mpaka 19. Sasa hapa tutajikita tu kuongezea nguvu zaidi katika uwekezaji, pengine tuje na programu za kimkakati zinazojikita zaidi kwenye masuala ya watoto wa kiume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani watoto walikuwa wanapelekwa jando, lakini sasa hivi tutakuwa tunapeleka jando

la kisasa na miongozo yao mizuri mizuri inayosema maana ya kuwa baba pindi wanapokuwa vijana balehe wajue changamoto watakayokutana nayo huko kwenye ndoa kwamba ndoa siyo mchezo, lakini itawezekana kwa sababu tumewaandaa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa mpango wa malezi na makuzi kwa mtoto ulishazinduliwa: Je, ni lini utekelezaji huu utaanza? Ahsante *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Suma, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu wa malezi na makuzi ya awali ya mtoto tulishauzindua tangu mwaka 2021, unakwenda mpaka 2026. Mojawapo ya afua zilizopo mle ni hizi za kujenga vituo hivi vya malezi na makuzi. Tayari vituo 200 vimeshajengwa kwenye maeneo mbalimbali ya jamii na sasa tunatafuta rasilimali na kuhamasisha jamii na wadau tuendelee kujenga kwenye maeneo ambayo yana hali mbaya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mpango huu unatekelezwa na tayari kuna watoto wapo humo wanapata hizi huduma na jamii imethibitisha kwamba kweli sasa hivi wazazi wanapata amani ya kwenda kutafuta maendeleo huku watoto wao wakiwa salama. Tutaongeza kasi hii na tutaleta taarifa kupitia Kamati zetu tunavyoendelea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru sana. Tunaendelea

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, sasa aulize swali lake.

Na. 44

**Ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji Mwibara**

**MHE. CHARLES M. KAJEGE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga skimu za umwagiliaji Kata za Kisorya, Igundu, Kwiramba, Namuhura, Butimba na Kasuguti - Mwibara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na zoezi la kubaini maeneo yote yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji nchini ili kuyapima na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kupata sgharama halisi za kutekeleza miradi hii kabla ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Tume imejipanga kuyafikia maeneo mbalimbali yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji nchini ikiwemo maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji yaliyopo ndani ya Jimbo la Mwibara ili kuingiza kwenye mpango wa utekelezaji, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza sikubaliani na majibu ya Serikali kwa sababu kila siku wanajipanga, wanajipanga;

wanafanya utafiti, wanafanya utafiti; sikubaliana nayo, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa vile Jimbo la Mwibara linakabiliwa na upungufu wa chakula na mojawapo ya sababu ikiwa ni ukosefu wa skimu za umwagiliaji maji: Je, ni lini Serikali itaanza tena mpango wa kupeleka chakula cha msaada katika Jimbo la Mwibara? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Serikali inaendelea kufanya kazi kulingana na mipango kama nilivyosema, katika mwaka wa 2023/2024 kuna fedha nyingi zimetengwa kwa ajili ya skimu za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na changamoto ya chakula katika Jimbo la Mwibara, utaratibu ni kwamba pale kunapokuwa na uhitaji wa msaada wa chakula katika maeneo husika, naomba viongozi ikiwemo kupitia Mbunge mweze kuandika barua ya maombi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu ili tuweze kuratibu namna ya kupeleka chakula cha msaada katika maeneo husika ili kufidia au kupunguza nakisi ya chakula na adha kwa wananchi katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na viongozi wengine ili kuandika barua na kupata maelekezo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali mwaka juzi 2021 ilitenga shilingi milioni 100 kupeleka Skimu ya Lwafi – Katangoro, lakini mpaka sasa hakuna tija yoyote imeonekana kwenye hiyo fedha: Ni upi mkakati wa Serikali wa kuongeza fedha ili kumaliza skimu hiyo na ianze kufanya kazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tayari katika mpango wa mwaka wa fedha huu tunaoenda nao, fedha nyingi zimewekwa kwa ajili ya kukamilisha skimu mbalimbali za miradi ambayo ni mipya na inayoendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe na imani kwamba sasa huu mradi utaenda kukamilishwa kwa sababu tayari fedha zimetengwa katika mwaka huu wa 2023/2024 ili kutekeleza pamoja na skimu nyingine ikiwemo na hiyo skimu ya kwa Mheshimiwa Aida Khenani, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Skimu za umwagiliaji wa maeneo ya chai kwenye Tarafa ya Igominyi katika Jimbo la Njombe Mjini: Nini kauli ya Serikali kuhusu utekelezaji katika kipindi hichi cha bajeti? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Skimu ya Igominyi na maeneo mengine kama alivyosema, ni skimu muhimu sana kwa ajili ya kuhakikisha kilimo cha chai kinaendelea kuchangia katika uchumi wa nchi. Ni nia ya Serikali kuona skimu zote ambazo ziko kwenye mpango wake zinatekelezwa. Kwa hiyo, fedha zitaendelea kupelekwa katika maeneo ambayo yamepangwa kulingana na mpango wa fedha katika mwaka wa fedha huu wa 2023/2024, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, tuna Skimu ya Udimaa na Skimu ya Ngaiti ambazo zimechakaa sana, lakini zipo kwenye bajeti ya mwaka huu: Je, ni lini Serikali itaanza utekelezaji wa kujenga hizi skimu mbili ambazo nimezitaja? Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni kweli tunajua katika baadhi ya maeneo skimu nyingi zimechakaa, kwa maana ni za muda mrefu. Ndiyo maana kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tayari tumeshaweka fedha kwenye mwaka huu wa 2023/2024. Kwa hiyo, muda wowote tutaanza kutekeleza skimu hizo ikiwemo ya kwa Mheshimiwa Mbunge kule Manyoni ili kuhakikisha skimu hizo zinaboreshwa ili ziweze kutoa faida kwa wakulima na kuweza kuhakikisha kilimo cha kisasa kinaendelea, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naipongeza sana Serikali kwa jitihada zake za kupanga mipango ya umwagiliaji. Kwa kuwa Serikali ndiyo yenye wataalam, wabobezi katika masuala haya ya umwagiliaji.

Je, ni lini Serikali itapanga mipango ya kuwasaidia wakulima kufanya *levelling* kufikisha maji kwenye mashamba yao badala ya kuwaachia kazi mkulima mmoja mmoja afanye jambo hilo ambapo hawana utaalamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inge-*copy* mambo yanayofanyika Egypt. Egypt wanafanyakazi zote mpaka kuwapeleka watu mashambani, kwa sababu ninyi ndio mna kamera, ninyi ndio mna vifaa vya kupimia: Sasa Serikali mna mpango gani wa kushughulikia wakilima ili maji yaende kwa watu wote?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni mawazo mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ndiYo yenye dhamana ya kuhakikisha skimu za umwagiliaji na kuhakikisha maji yanaenda katika mashamba na maeneo mbalimbali ambako wananchi wanafanya shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango ya Serikali tumesema moja ya maeneo ambayo yameongezwa sana fedha ni kwenye maeneo haya ya umwagiliaji. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mipango ya Serikali ni thabiti na itaendelea kutekelezwa kulingana na fedha ambazo tunazipanga na kuhakikisha tunaenda na vipaumbele katika maeneo ambayo kuna mahitaji haya ya skimu za umwagiliaji. Hivyo, tuwaondoe hofu Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba Serikali itatekeleza miradi yake na mipango yake kwa kadri ambavyo tunapanga kwenye mipango ya kila mwaka wa fedha wa bajeti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Skimu ya Bukangilija na Masela ni lini itaanza kujengwa Wilaya ya Maswa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, skimu zote ambazo ziko kwenye mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 na pia hata hizo mpya ambazo tunaendelea kuzipata zitawekwa kwenye mipango ya bajeti na hivyo zitajengwa kwa kadri ambavyo tumepangia kwenye mipango yetu ya Serikali pamoja na skimu aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, nayo pia

itaweza kufanyiwa kazi kadri ambavyo Serikali itakuwa imejipanga, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Kijiji cha Makangaga, Kata ya Kiranjeranje Jimbo la Kilwa Kusini, kuna skimu ya umwagiliaji ambayo imetelekezwa kwa muda mrefu: Je, Serikali ipo tayari kupeleka wataalamu pale Makangaga ili wakafanye upembuzi yakinifu na hatimaye skimu hii iweze kufufuliwa mara moja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Serikali itapeleka wataalam waweze kutathmini hiyo skimu na kuona gharama na mahitaji halisi ili iweze kuboreshwa na iweze kutoa tija kwa wakulima wanaotumia skimu hiyo, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mkoa wa Rukwa, Wilaya ya Kalambo, Tarafa ya Mwimbi kuna mito mingi sana ya kutosha: Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika tarafa hiyo? Ahsante *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Azma ya Serikali ni kutumia vyanzo vyote vya maji vilivyopo, ikiwemo mito ambayo ni muhimu sana kwa ajili ya kuhakikisha skimu za umwagiliaji zinafanya kazi. Kwa hiyo, katika maeneo ambayo tutaendelea pia kuyafanyia kazi ni mito hiyo iliyopo katika Jimbo

la Kalambo ili kuhakikisha nayo inatumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika eneo husika ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali ilishachukua vipimo vya kujenga Bwawa la Iyongoma na bwawa hili ni muhimu sana kwa ajili ya kumwagilia Skimu ya Ndungu ambayo kwa muda mrefu imekuwa na matatizo: Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga bwawa hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo yeye mwenyewe amesema kwamba tayari kuna mipango inaendelea kuhakikisha tunalijenga hilo bwawa na wataalamu kama walishakuja kuangalia. Moja ya maeneo ambayo tutaangalia ni haya ambayo tayari yameshafanyiwa usanifu yakinifu ili yaweze kuanza kutekelezwa kadiri ambavyo tumepanga kwenye bajeti zetu za Wizara na kuhakikisha pia kama kuna miradi mingine ambayo itapelekea kukamilisha mabwawa haya nayo pia tutaangalia. Kwa hiyo, hili bwawa nalo litawekwa katika kipaumbele katika mipango ya Wizara, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Najua Wizara siyo yako, lakini umefanya kazi kubwa, tunakupongeza, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu asubuhi hii. Yako matangazo machache mbele yetu. Tangazo la kwanza ni wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Kwanza ni wageni waliopo Jukwaa la Spika; tunaye mgeni wa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara ambaye ni Katibu MKuu wa Wizara hiyo, Dkt. Hashil Abdallah, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tuna wageni 52 wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni wanafunzi na walimu wa *Ethics Pre and Primary School* kutoka Mafinga, Mkoani Iringa. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Vedatus Mathayo kutoka *UDOM*. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Mariam Omari ambao ni familia yake kutoka Pandani, Kaskazini Pemba, Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wageni 54 na walimu sita kutoka Shule ya Msingi ya Tuishime iliyoko Njiro, Jijini Arusha. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 60 na walimu nane wa Shule ya Sekondari ya Wasichana *St. Ursual* kutoka Mtumba, Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunaye Ndugu Chuma R. Chuma ambaye ni mfanyakazi wa *Azam Media Ltd.* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana na ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMO

### Azimio la Bunge kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya Mwaka 2012 *(SADC Protocol on Trade in Services, 2012)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge tunamwita sasa mtoa hoja ambaye ni Waziri wa Viwanda na Biashara kwa ajili ya Azimio lililopo mbele yetu. Mheshimiwa Waziri, karibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kunipa kibali kwa mara nyingine tena cha kuhudumu kwenye Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Naomba pia nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara ili niweze kuhudumia Watanzania kwenye *portfolio* hii. Mimi pamoja na wenzangu tunamuahidi Mheshimiwa Rais wetu utumishi unaozingatia weledi na uadilifu wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kuwasilisha jukumu lililo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(Southern African Development Community)* ilianzishwa mwaka 1992 kutoka katika iliyokuwa Jumuiya ya Kuratibu Mikutano ya Shughuli za Kimaendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika iliyoanzishwa mwaka 1980 kwa lengo la kutafuta ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika. Baada ya kukamilika kwa lengo la ukombozi, malengo ya Jumuiya yalibadilika na kujikita katika matumizi bora ya rasilimali na kujitegemea, kukuza uchumi, kupunguza umaskini, na kuimarisha ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Jumuiya ina nchi wanachama 16 ambazo ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Angola, Afrika Kusini, Botswana, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Shelisheli, Eswatini, Zambia na Zimbabwe. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilijiunga na *SADC* kupitia Azimio la Bunge lililopitishwa tarehe 27 Agosti, 1993 na hati iliyowasilishwa Sekretarieti ya Jumuiya hiyo mnamo tarehe 5 Septemba, 1993 ikiridhia uanachama wa Tanzania katika kanda hiyo ya *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukuza mtangamano wa kiuchumi miongoni mwao nchi wanachama zilisaini Itifaki ya biashara ya *SADC* tarehe 24 Agosti, 1996 Maseru - Lesotho na kuanza utekelezaji wake mwezi Januari, 2000. Lengo la Itifaki hiyo ni pamoja na kurahisisha ufanyaji biashara ya bidhaa na huduma miongoni mwa nchi wanachama kupitia uondoaji wa vikwazo vya kibiashara kuondoa ushuru wa forodha kwenye bidhaa zinazokidhi vigezo vya uasili wa bidhaa na kuwianisha sera za biashara kulingana na viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 23 ya Itifaki ya biashara ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC Protocol on Trade)* inaelekeza kuanzishwa Itifaki ya Biashara ya Huduma *(Protocol on Trade and Services)*. Katika kutekeleza suala hilo, wakuu wa nchi na Serikali wa *SADC* walisaini Itifaki ya Biashara ya Huduma tarehe 18 Agosti, 2012 Maputo – Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 29 ya Itifaki hiyo ya biashara ya ya huduma ya *SADC* inazitaka nchi wanachama kuridhia Itifaki hiyo kulingana na taratibu zao za ndani. Aidha hadi sasa jumla ya nchi wanachama 11 kati ya 16 sawa na 2/3 ya nchi wanachama wa *SADC* zilikuwa tayari zimesharidhia Itifaki hiyo na kuipa nguvu ya kisheria kuanza ketekelezwa. Nchi ambazo hazijaridhia Itifaki hiyo ni Tanzania, Angola, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Madagascar na Comoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Itifaki ya Biashara ya Huduma kusainiwa, nchi wanachama zilianza awamu ya kwanza

ya majadiliano ya ulegezaji wa masharti ya biashara ya huduma. Majadiliano hayo yalihusisha sekta sita za kipaumbele ambazo ni mawasiliano, fedha, utalii, uchukuzi, nishati na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hizo zilichaguliwa kwa kuzingatia mchango wake katika maendeleo ya chumi za nchi wanachama na kiwango cha mtangamano baina ya nchi wanachama katika sekta hizo. Awamu ya pili ya majadiliano yanahusisha sekta sita zilizosalia ambazo ni huduma za biashara, usambazaji, elimu, mazingira, afya ya jamii, burudani na utamaduni na michezo. Majadiliano haya bado yanaendelea na Serikali inashiriki kikamilifu kwa kushirikiana na wadau wengine muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendelea kuimarisha mtangamano na fursa za biashara hususani biashara ya huduma kwenye kanda ya *SADC* na kitaifa, Serikali imeona ni muhimu kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya mwaka 2012. Kuridhiwa kwa Itifaki hiyo ni moja ya nyenzo muhimu katika kuifanya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kuimarika katika mtangamano wake wa kibiashara na uchumi na hivyo kupanua fursa zaidi za biashara ya huduma miongoni mwa nchi wanachama ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukubalika kwa hoja hii kutatoa fursa na manufaa kwa nchi kama ifuatavyo:-

(a) Kupatikana kwa soko kubwa la bidhaa na huduma lenye idadi ya watu takribani milioni 360 katika Jumuiya ya *SADC;*

(b) Kuongezeka kwa tija na ubora wa bidhaa na huduma za Tanzania kutokana na kuongezeka kwa ushindani na hivyo kupelekea kupungua kwa gharama za kupata huduma;

(c) Upatikanaji wa bidhaa za huduma za aina mbalimbali ndani ya nchi yetu na;

(d) Uhaulishaji wa teknolojia kutoka nje ya nchi kutokana na uwekezaji utakaofanyika nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa maeneo ya Sekta ya Huduma ambayo Taifa letu limepiga hatua na linaendelea kukua ni pamoja na uwekezaji kwenye miundombinu ya usafirishaji, mawasiliano, huduma za kifedha, utalii, huduma za bima, afya na nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya mwaka 2012 kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kupitia Azimio la Bunge lililopitishwa tarehe 27 Agosti, 1993 na hati iliyowasilishwa Sekretariet ya Jumuiya hiyo mnamo tarehe 5 Septemba, 1993.

Na kwa kuwa kwa kutambua malengo yaliyomo kwenye mkataba wa uanzishwaji wake, wakuu wa nchi na Serikali wa Jumuiya ya Kusini mwa Afrika ikiwemo Tanzania kupitia mkutano wao uliofanyika Mjini Maputo – Msumbiji walisaini Itifaki ya Biashara ya Huduma mwezi Agosti mwaka 2012 ambayo inalenga kuchochea uchumi na biashara miongoni mwa nchi wanachama kwa kufunguliana masoko ya biashara ya huduma kwa lengo la kuondoleana vikwazo na kulegezeana masharti na taratibu mbalimbali za utoaji huduma.

Na kwa kuwa itifaki hiyo ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ilianza kutumika tangu tarehe 13 Januari, 2022 baada ya kuridhiwa na 2/3 ya nchi wanachama wa *SADC* ambapo nchi tano wanachama bado hazijaridhia Itifaki hiyo zikiwemo Tanzania, Angola, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Madagascar na Comoro.

Na kwa kuwa Tanzania ikiwa miongoni mwa nchi zilizosaini Itifaki hiyo inapaswa kuridhia Itifaki hiyo ili iweze kunufaika na

ushirikiano katika biashara ya huduma katika kukuza biashara ya bidhaa na kutekeleza malengo mapana ya *SADC* ya kukuza na kuondoa umasikini.

Na kwa kuwa kuridhiwa kwa Itifaki hii ni moja ya nyenzo muhimu katika kuifanya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kuimarika katika mtangamano wake wa kibiashara na uchumi.

Na kwa kuwa madhumuni na misingi ya uanzishwaji wa Itifaki hii ya Biashara ya Huduma ni pamoja na:-

(i) Kuendelea kufunguliana fursa miongoni mwa nchi wanachama katika biashara ya huduma katika Jumuiya kwa msingi wa usawa na manufaa ya pande zote kwa lengo la kuondoa upendeleo miongoni mwa nchi wanachama na kuweka mfumo mzuri wa biashara huria wa biashara ya huduma kwa lengo la kuunda soko moja la biashara ya huduma katika Jumuiya;

(ii) Kukuza ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu na hivyo kuinua viwango na ubora wa maisha ya watu wa nchi wanachama na kupunguza umasikini kupitia ushirikiano wa kikanda katika eneo la huduma;

(iii) Kuimarisha maendeleo ya kichumi, kitaifa, kikanda na kuvutia uwekezaji kutoka nje katika maendeleo ya kiuchumi kupitia uwekezaji wa ndani kikanda na kimataifa katika kuharakisha maendeleo ya chumi za nchi wanachama kupitia sekta ya huduma;

(iv) Kuhakikisha uwiano kati ya biashara huria ya huduma na Itifaki mbalimbali katika sekta mahususi za huduma unakuwepo;

(v) Kusimamia jukumu la ufunguaji wa biashara ya huduma huku ikizingatiwa kikamilifu haki ya kudhibiti na kuanzisha kanuni mpya na

(vi) Kuimarisha uwezo na ushindani wa sekta za huduma za nchi wananachama.

Na kwa kuwa kwa kuridhia Itifaki hii, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata manufaa yafuatayo:-

(a) Kupatikana kwa soko kubwa la bidhaa na huduma lenye idadi ya watu takribani milioni 360 katika Jumuiya ya *SADC;*

(b) Kuongezeka kwa tija na ubora kwa bidhaa na huduma za Tanzania kutokana na kuongezeka kwa ushindani na hivyo kupelekea kupungua kwa gharama za kupata huduma;

(c) Upatikanaji wa bidhaa za huduma za aina mbalimbali nchini na;

(d) Uhaulishaji wa teknolojia kutoka nje ya nchi kutokana na uwekezaji utakaofanyika nchini.

Hivyo basi kwa kuzingatia manufaa hayo ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itapata kutokana na kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya mwaka 2012. Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Kumi na Moja na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 linaazimia kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya mwaka 2012 *(SADC Protocol on Trade and Services 2012)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri na hoja imeungwa mkono, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa niaba yake Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile, karibu.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Azimio la Bunge kuhusu mapendekezo ya kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya mwaka 2012 *(SADC Protocol on Trade and Services 2012)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 60(6)(b) ikisomwa pamoja na kifungu cha 1(a,b,c) cha nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023. Naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna Kamati ilivyofanya kazi. Baada ya kupokea maelekezo ya kulishughulikia jambo hili kwa mujibu wa kanauni ya 108(1) na (2) Kamati ilianza kazi mara moja na kufanya yafuatayo:-

(a) Kufanya uchambuzi wa awali na baadaye kupokea maelekezo ya Serikali kuhusu mapendekezo ya Azimio la kuridhia Itifaki husika ambapo kazi hii ilifanyika siku ya Jumatatu tarehe 21 Agosti, 2023;

(b) Kupokea na kuchambua maoni ya wadau yaliyowasilishwa mbele ya Kamati siku ya Ijumaa tarehe 25 Agosti, 2023. Aidha, Kamati ilipokea maoni yaliyowasilishwa kwa njia ya mtandao ambapo mpaka wakati kamati inakamilisha kazi yake ilipokea maoni kutoka kwa jumla ya wadau wanne; na

(c) Kufanya uchambuzi wa Itifaki husika kwa kuzingatia uchambuzi wa awali, maelekezo ya Serikali pamoja na maoni ya wadau yaliyowasilishwa kwa njia mbalimbali ambapo kazi hii ilifanyika kuanzia tarehe 26 hadi 28 Agosti, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilipata nafasi ya kufanya tathmini ili kupima iwapo kuna manufaa au athari ambazo Tanzania inaweza kuzipata ikiwa Bunge litaridhia Itifaki hii kwa mujibu wa kanuni ya 107(2)(f) na (g).

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Itifaki. Msingi wa Itifaki ya Biashara ya Huduma kwa nchi wanachama wa *SADC* unatokana na Itifaki ya Biashara ya *SADC* ya mwaka 1996 *(SADC Protocol on Trade 1996)* ambapo tarehe 18 Agosti, 2012 wakuu wa nchi wanachama na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ikiwemo Tanzania kupitia mkutano uliofanyika Jijini Maputo - Msumbiji walisaini Itifaki ya Biashara ya Huduma. Itifaki hiyo inalenga kufungua masoko ya biashara ya huduma kwa lengo la kuondoa vikwazo na kulegeza masharti na taratibu mbalimbali za utoaji huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki hii ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ilianza kutumika tarehe 13 Januari, 2022 baada ya kuridhiwa na 2/3 ya nchi wanachama wa *SADC*. Aidha, hadi sasa nchi tano wanachama hazijaridhia Itifaki hiyo ambazo ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Angola, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo *(DRC),* Madagascar na Comoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati; msingi wa uchambuzi. Hoja iliyowasilishwa na Serikali inapendekeza Bunge lako Tukufu liridhie Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ya mwaka 2012 *(SADC Protocol on Trade and Services 2012)* ili kutimiza masharti ya Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 imeweka utaratibu wa Bunge kujadili hoja ya kuridhia mikataba ya kimataifa ambao unaitaka Serikali kuwasilisha hoja yake Bungeni pamoja na Itifaki inayokusudiwa kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawanda ya uchambuzi. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kupitia ibara zote za Itifaki ili kupata uelewa wa kutosha kuhusu masharti yaliyomo pamoja na maudhui yake; aidha, Kamati ilipitia maelezo ya taarifa ya Serikali pamoja na maoni ya ushauri wa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya uchambuzi wa Itifaki hii, Kamati pia ilizingatia masharti ya Kanuni ya 107(2) ya Kanuni za Bunge yanayotokana na uchambuzi kuzingatia yafuatayo:-

(a) Wajibu na haki za wananchi baada ya kusaini Itifaki;

(b) Uzingatiaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 katika Itifaki;

(c) Manufaa ambayo Tanzania itapata kutokana na Itifaki hii;

(d) Athari ambazo zinaweza kutokana na Itifaki hii na;

(e) Jambo lingine lenye tija kwa Taifa kutokana na makubaliano husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa maelezo ya taarifa ya Serikali, maoni na ushauri wa wadau pamoja na uchambuzi wa kina wa Kamati vimejenga msingi ambao utalisaidia Bunge lako Tukufu katika kuridhia Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya msingi yaliyozingatiwa na Kamati katika uchambuzi. Katika uchambuzi wake, Kamati

ilizingatia katika kujua aina ya Itifaki inayokusudiwa kuridhiwa na Serikali ili kujiridhisha kikamilifu kuhusiana na lengo, madhumuni, mawanda na manufaa tarajiwa ya Itifaki hii. Itifaki hii ni baina ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* ambapo Tanzania ni mwanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Itifaki. Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu lengo hasa la Itifaki na endapo likiridhia haitaathiri biashara ya huduma inayofanywa na wananchi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la Itifaki hii ni kuendeleza kutekeleza malengo mapana ya *SADC* ya kukuza mtangamano wa kiuchumi na kuondoa umasikini miongoni mwa nchi wanachama kwa kufungua masoko ya biashara ya huduma ili kuondoa vikwazo na kulegeza masharti na taratibu mbalimbali za utoaji huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawanda ya utekelezaji wa Itifaki. Kamati ilitaka kupata uelewa wa maeneo yatakayoguswa na Itifaki hii na kujiridhisha iwapo maeneo hayo yana manufaa kwa Taifa na kwamba Taifa halitageuka kuwa soko kwa huduma mbalimbali za nchi wanachama wa *SADC* na kuwaacha Watanzania bila ya kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki hii inahusisha jumla ya sekta 12 ambapo nchi wanachama zilianza awamu ya kwanza ya majadiliano ya ulegezaji wa masharti ya biashara ya huduma, majadiliano hayo yanahusisha sekta sita za kipaumbele ambazo ni; mawasiliano, fedha, utalii, uchukuzi, nishati na ujenzi. Sekta hizi zilichaguliwa kwa kuzingatia mchango wake katika maendeleo na kiwango cha mtangamano baina ya nchi wanachama ambazo ni Tanzania, Afrika Kusini, Zambia, Lesotho, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Zimbabwe, Malawi, Eswatini, Namibia, Angola, Botswana, Msumbiji, Mauritania, Shelisheli, Comoro na Madagascar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile awamu ya pili inahusisha sekta sita zilizosalia ambazo ni usambazaji, elimu, mazingira, afya ya jamii, burudani na utamaduni na michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kutathmini kwa kina kuhusu sekta zinazoridhiwa na Itifaki hii, Kamati imejiridhisha kuwa nchi yetu iko kwenye nafasi nzuri ya kunufaika na biashara ya huduma katika sekta hizo kwenye soko la *SADC* ikiwa Serikali itatekeleza wajibu wake wa kuendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara ya huduma hii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali, kuridhia Itifaki na kutatoa fursa na manufaa yafuatayo kwa Taifa: -

a) Biashara na bidhaa zinazoendana na huduma zinazozalishwa na kutolewa nchini zitalifikia soko la *SADC* lenye idadi ya watu zaidi ya milioni 360.

b) Kuongezeka kwa uwekezaji nchini, kuvutia mitaji kutoka nje yaani foreign *capital,* kukuza ushiriki wa wananchi katika kutoa huduma na kuongeza Pato la Taifa.

c) Kuongezeka kwa fursa za ajira.

d) Kuongezeka kwa ufanisi na ubora wa huduma.

e) Kuwepo kwa unafuu wa gharama za upatikanaji wa huduma katika sekta zitakazofunguliwa kutokana na ushindani.

f) Kukua kwa mitaji ya wawekezaji wa ndani kupitia ubia na wawekezaji kutoka nchi wanachama na wale wasio wanachama; na

g) Kukua kwa teknolojia na utaalam kupitia uhaulishwaji kutoka nchi wanachama na wale wasio wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa hizi zinazoambatana na kuridhia Itifaki zinatoa nafasi kubwa kwa Taifa letu kunufaika na itifaki ikiwa Serikali itaendelea kuboresha mifumo itakayovutia na kuboresha mazingira kisera, kisheria na kiusimamizi ya ufanyaji biashara ya huduma. Ni dhahiri kuwa kwa kuridhia Itifaki hii, Tanzania sasa itakuwa katika nafasi nzuri ya kuonesha fursa zake za kibiashara ikiwa ni pamoja na kueneza utamaduni wake kwa nchi wanachama kwa kuzingatia kuwa Kiswahili kimekuwa miongoni mwa lugha kuu nne zinazotumika katika shughuli za nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hangamoto zinazoweza kukwamisha manufaa ya Itifaki, kutokana na uchambuzi wa Kamati, imebainika kwamba zipo changamoto kadhaa zinazoweza kukwamisha ama kucheewesha nchi yetu kunufaika ipasavyo na Itifaki hii. Changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa taarifa na elimu ya kutosha kuhusu fursa za biashara ya huduma zinazopatikana miongoni mwa nchi wanachama wa *SADC*, wananchi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, uwepo wa sera, sheria na kanuni zilizopitwa na wakati zinazosimimia sekta ya biashara nchini. Naomba kurudia. Uwepo wa sera, sheria na kanuni zilizopitwa na wakati zinazosimimia sekta ya biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kujadiliana na Serikali kuhusu changamoto hizo na kukubaliana kwa pamoja kwamba utatuzi wa changamoto hizi utasaidia katika kuongeza manufaa ambayo nchi yetu inaweza kuyapata kutokana na kuridhiwa kwa Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; Kamati imefanya uchambuzi wake na kukamilisha, hivyo kuwasilisha Bungeni ili kuliwezesha Bunge lako tukufu kutekeleza Ibara ya 63, ibara ndogo ya 3 (e) ya Katiba na pia kuiwezesha Serikali kuendelea na taratibu zingine za kuridhiwa kwa Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inaona ipo haja ya Serikali kuzingatia maoni na ushauri ufuatao kwa lengo la

kuboresha mazingira ya utekelezaji wa Itifaki ya Biashara ya Huduma na kuleta tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

(a) Sera, sheria na kanuni za biashara zilizopitwa na wakati, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inakamilisha mapitio ya sera, sheria na kanuni za biashara zilizopitwa na wakati ili kuendana na mahitaji ya sasa ya biashara hasa ukuaji wa sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa sera na sheria hizo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Uhamasishaji wa Uwekezaji ya mwaka 1996, Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003, Sheria ya Kujilinda dhidi ya Athari za Kibiashara yaani *Trade Remedies Act* ya 2021, Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 na Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003. Aidha, Serikali iboreshe mifumo ya usimamizi na uratibu wa shughuli za kibiashara ili kuleta ufanisi katika kutekeleza Biashara ya Huduma.

(b) Ushirikishwaji wa sekta binafsi, kwa kuwa Sekta binafsi ina mchango mkubwa katika uwekezaji wa biashara ya huduma hapa nchini, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhakikisha Serikali inaishirikisha kikamilifu sekta binafsi katika hatua zote za utekelezaji wa Itifaki hii, ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo na uelewa wa fursa za kibiashara ili washiriki ipasavyo na kurahisisha utekelezaji wake katika kutumia fursa zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iweke mfumo na mkakati madhubuti wa kuhakikisha wafanyabiashara wanashiriki ipasavyo katika kuzitumia fursa zilizopo kwenye Itifaki hii na kunufaika nazo na Iboreshe mifumo iliyopo ya utoaji leseni za biashara ili isiwe kikwazo kwenye Biashara ya Huduma.

(c) Chombo cha kutatua migogoro, kwa kuwa ufanyaji wa biashara mara nyingi huwa na migogoro inayohusisha ushuru na vikwazo visivyokuwa vya kiushuru, Kamati inashauri kwamba, ni muhimu kuanzisha chombo kitakachosimamia masuala ya

kutatua migogoro ya kibiashara mara tu baada ya Itifaki kuanza kutekelezwa badala ya kusubiri hadi mgogoro utakapoibuka.

(d) Mazingira ya ufanyaji biashara. Ili Itifaki hii iweze kuleta tija inayotarajiwa kwa nchi yetu, Kamati inashauri Serikali yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, iendelee kuboresha na kujiimarisha katika maeneo yote yanayotumika kama kichocheo cha biashara kama vile sera, sheria na kanuni zinazosimamia masuala ya ushindani. Kuboresha usimamizi katika sekta zinazohusu biashara za huduma na kuimarisha miundombinu ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kuimarisha huduma za kimtandao Kwa kuwa dunia inakabiliwa na uhalifu wa kimtandao unaoweza kuleta tishio kubwa kwa usalama wa nchi, mashambulizi dhidi ya Serikali na kuathiri mifumo, habari nyeti na upotevu wa fedha au mapato. Ni ushauri wa Kamati kuwa, ili kuepukana na changamoto hiyo Serikali ihakikishe kuna kuwa na ulinzi wa kutosha kwenye mifumo ya kimtandao nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuweka mazingira mazuri yatakayovutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini na kuingiza fedha za kigeni. Kwa mfano, hivi sasa matengenezo ya meli na ndege yanafanyika nje ya nchi hali inayochangia kutumia kiasi kikubwa cha fedha za kigeni. Ni wakati sasa wa kuvutia wafanyabiashara ya huduma ya kuja kuwekeza kwa kujenga karakana za ndege na meli zitakazosaidia kufanya matengenezo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zinazoikabili sekta ya usafiri, kwa kuwa ipo changamoto ya madereva wa malori kuzuiliwa kupita katika baadhi ya mipaka ya nchi za *SADC*, hali inayopelekea bidhaa kuharibika, Kamati inaiomba Serikali kuhakikisha changamoto hii inatatuliwa ili isiwe kikwazo kwenye utekelezaji wa Itifaki ya Biashara ya Huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya amani katika utekelezaji wa Itifaki, kwa kuwa imewahi kutokea kwa baadhi ya nchi wanachama *SADC* ikiwemo Afrika ya Kusini kuanzisha vurugu dhidi ya raia wa nchi zingine ambao ni wananchi wa *SADC (Zenophobia)*, hali iliyopelekea vifo, uharibifu wa mali na miundombinu, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha raia wote wanalindwa ilimradi hawakiuki sheria na taratibu za nchi wanachama ili waweze kutekeleza shughuli zao kama malengo ya Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutumia fursa za umahiri zilizopo kwenye Itifaki *(comparative advantage),* kwa kuwa Tanzania iko katika nafasi nzuri ya kunufaika na Itifaki hii kulinganisha na nchi nyingine, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatumia vizuri uwepo wa Itifaki katika kupeleka huduma katika nchi wananchama wa *SADC*, hivyo kuvutia mitaji zaidi kutoka nje na mfano wa fursa hizo ni: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa nishati ya ziada, kwa kuwa ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere hadi kufikia tarehe 31 Julai, 2023 umeshafikia 90.19% na kwa kuwa mradi huo ukikamilika nchi itakuwa na umeme wa ziada, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali itumie fursa iliyopo katika Itifaki hii ili kuuza umeme katika nchi za wanachama wa *SADC* ambao wa upungufu wa bidhaa hiiya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za afya, kwa kuwa huduma za afya nchini zimeendelea kuboreshwa na Tanzania imejipanga kuleta utalii wa kitabibu, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali iweke mikakati ya kuimarisha huduma hizo ili kuvutia nchi wanachama kuja kutibiwa katika hospitali zetu, hali itakayochangia ongezeko la fedha za kigeni. Vilevile, madaktari kutoka nchini wapate fursa ya kubadilishana uzoefu na nchi wanachama wa *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuzaji wa Sekta ya Utalii, kwa kuwa Itifaki itaruhusu uwekezaji wa hoteli za kitalii katika nchi Wanachama na kwa kuwa nchi yetu ilishaweka viwango vya ujenzi kuanzia nyota nne na kuendelea, Kamati inaishauri Serikali

kuhakikisha vigezo vilivyowekwa vinafuatwa badala ya kujenga kiholela na kuharibu mandhari ya maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa sekta ya elimu, kwa kuwa Tanzania tuna wahitimu katika fani mbalimbali ikiwemo waliohitimu shahada ya Lugha ya Kiswahili na kwa kuwa kuna fursa ya kufundisha katika nchi mbalimbali Wanachama wa *SADC*, Kamati inaishauri Serikali kutumia Itifaki hii kutangaza Lugha ya Kiswahili ili kuongeza ajira kwa walimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyotimiza majukumu yenu kwa weledi na umakini mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa ushirikiano wao na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha kushughulikia Azimio hili, kwa kweli hapa niwapongeze sana Wajumbe kwani hata siku ambazo si za kazi tulikuwa tunakutana kwa ajili ya kuchakata jambo hili na hatukusita katika kuhakikisha linafanikiwa kwa ufanisi mkubwa sana. Nawapongeza sana Wajumbe wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia ufinyu wa muda tulionao naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo; laikini pia kuingia kwenye *Hansard,* kama, muda unaniruhusu basi naomba majina yote yaingie kwenye kumbukumbu ya *Hansard.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati natumia fursa hii kumshukuru kwanza Waziri wa Viwanda na Biashara ambaye pia ni Mbunge wa Kondoa Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji Kachwamba almaarufu Kamsese pamoja na Naibu Waziri Exaud Kigahe Mbunge wa Mufindi na watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Hashil Abdallah kwa ushirikiano

wao kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, kwanza tunapenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumuona miongoni mwa Wajumbe wa Kamati, Mwenyekiti wetu na kumpa heshima ya kumteua kuwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa niaba ya Kamati tunapenda sana kumshukuru Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii na ama hakika alituongoza kwa moyo mmoja na umakini mkubwa hadi kufikia jana tarehe 30 Agosti, 2023 kwa uongozi wake mahiri kwa kipindi chote alichokuwa akiongozi wa Kamati yetu. Tunampongeza sana na tunamtakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yake mapya ya Unaibu Waziri wa Uchukuzi. *(Makofu)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ama hakika kwangu binafsi amekuwa mwalimu mzuri sana kwangu mimi kama Makamu Mwenyekiti wake na hakika ameweza kunitengeneza vizuri na Wajumbe wanalitambua hilo. Mwisho lakini siyo kwa umuhimu namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi kwa kuwaongoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Azimio, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**31 AGOSTI, 2023**

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU AZIMIO LA BUNGE KUHUSU MAPENDEKEZO YA KURIDHIA ITIFAKI YA BIASHARA YA HUDUMA YA JUMUIYA YA MAENDELEO KUSINI MWA AFRIKA YA MWAKA 2012 (SADC PROTOCOL ON TRADE IN SERVICES, 2012) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 60(6) (b), ikisomwa pamoja na Kifungu cha 6(1) (a, b, c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika ya Mwaka 2012 (SADC Protocol on Trade in Services, 2012).

### 1.2 Namna Kamati ilivyofanya Kazi

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupokea maelekezo ya kulishughulikia jambo hili kwa mujibu wa **Kanuni ya 108 (1) na (2)**, Kamati ilianza kazi mara moja na kufanya yafuatayo:-

(a) Kufanya uchambuzi wa awali na baadae kupokea maelezo ya Serikali kuhusu mapendekezo ya Azimio la Kuridhia Itifaki husika ambapo kazi hii ilifanyika siku ya Jumatatu tarehe 21 Agosti, 2023;

(b) Kupokea na kuchambua maoni ya wadau yaliyowasilishwa mbele ya Kamati siku ya Ijumaa tarehe 25 Agosti, 2023. Aidha, Kamati ilipokea maoni yaliyowasilishwa kwa njia ya mtandao ambapo mpaka wakati Kamati inakamilisha kazi yake ilipokea maoni kutoka kwa jumla ya wadau wanne (4);

(c) Kufanya uchambuzi wa Itifaki husika kwa kuzingatia uchambuzi wa awali, maelezo ya Serikali pamoja na maoni ya Wadau yaliyowasilishwa kwa njia mbalimbali ambapo kazi hii ilifanyika kuanzia tarehe **26 hadi 28 Agosti, 2023.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilipata nafasi ya kufanya tathmini ili kupima iwapo kuna manufaa au athari ambazo Tanzania inaweza kuzipata ikiwa Bunge litaridhia Itifaki hii kwa mujibu wa **Kanuni ya 107 (2) (f)** na **(g).**

**1.3 Chimbuko la Itifaki**

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa Itifaki ya Biashara ya Huduma kwa nchi Wanachama wa SADC, unatokana na Itifaki ya Biashara ya SADC ya Mwaka 1996 (SADC Protocol on Trade 1996) ambapo, tarehe 18 Agosti, 2012 Wakuu wa nchi Wanachama na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ikiwemo Tanzania kupitia mkutano uliofanyika jijini Maputo Msumbiji walisaini Itifaki ya Biashara ya Huduma.

**Mheshimiwa Spika**, Itifaki hiyo inalenga kufungua masoko ya biashara ya huduma kwa lengo la kuondoa vikwazo na kulegeza masharti na taratibu mbalimbali za utoaji huduma.

**Mheshimiwa Spika**, Itifaki hii ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ilianza kutumika tarehe 13 Januari, 2022 baada ya kuridhiwa na theluthi mbili ya nchi wanachama wa SADC. Aidha, hadi sasa nchi tano wanachama hazijaridhia Itifaki hiyo ambazo ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Angola, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Madagascar na Comoro.

**SEHEMU YA PILI**

**2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI**

**2.1 Msingi wa Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika,** hoja iliyowasilishwa na Serikali inapendekeza Bunge lako Tukufu liridhie Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini Mwa Afrika ya Mwaka 2012 (SADC Protocol on Trade in Services, 2012) ili kutimiza masharti ya Ibara

ya **63 (3) (e)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 107 (1)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 imeweka utaratibu wa Bunge kujadili hoja ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa ambao unaitaka Serikali kuwasilisha hoja yake Bungeni pamoja na Itifaki inayokusudiwa kuridhiwa.

**2.2 Mawanda ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kupitia Ibara zote za Itifaki ili kupata uelewa wa kutosha kuhusu masharti yaliyomo pamoja na maudhui yake. Aidha Kamati ilipitia maelezo ya Taarifa ya Serikali pamoja na Maoni na Ushauri wa Wadau.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanya uchambuzi wa Itifaki hii, Kamati pia ilizingatia masharti ya **Kanuni ya 107 (2**) ya Kanuni za Bunge inayotaka uchambuzi kuzingatia yafuatayo:-

a) Wajibu na Haki za Wananchi baada ya kusaini ifitaki;

b) Uzingatiaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 katika Itifaki;

c) Manufaa ambayo Tanzania itapata kutokana na itifaki hii;

d) Athari ambazo zinaweza kutokana na Itifaki hii; na

e) Jambo lingine lenye tija kwa Taifa kutokana na makubaliano husika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, maelezo ya Taarifa ya Serikali, Maoni na Ushauri wa Wadau Pamoja na uchambuzi wa kina wa Kamati, vimejenga msingi ambao utalisaidia Bunge lako Tukufu katika kuridhia Azimio hili.

## 2.3 Masuala ya Msingi Yaliyozingatiwa na Kamati katika Uchambuzi

### 2.3.1 Aina ya Itifaki

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilizingatia kutaka kujua aina ya Itifaki inayokusudiwa kuridhiwa na Serikali ili kujiridhisha kikamilifu kuhusiana na lengo, madhumuni, mawanda na manufaa tarajiwa ya Itifaki hii.

**Mheshimiwa Spika,** Itifaki hii ni baina ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ambapo Tanzania ni Mwanachama.

### 2.3.2 Lengo la Itifaki

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu lengo hasa la Itifaki na endapo Bunge likiridhia haitaathiri biashara ya huduma inayofanywa na wananchi wa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la Itifaki hii ni kuendelea kutekeleza malengo mapana ya SADC ya kukuza mtangamano wa kiuchumi na kuondoa umaskini miongoni mwa nchi wanachama kwa kufungua masoko ya biashara ya huduma ili kuondoa vikwazo na kulegeza masharti na taratibu mbalimbali za utoaji huduma.

### 2.3.3 Mawanda ya Utekelezaji wa Itifaki

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kupata uelewa wa maeneo yatakayoguswa na Itifaki hii na kujiridhisha iwapo maeneo hayo yana manufaa kwa Taifa na kwamba Taifa halitageuka kuwa soko kwa huduma mbalimbali za nchi wanachama wa SADC na kuwaacha Watanzania bila kunufaika.

**Mheshimiwa Spika,** Itifaki hii inahusisha jumla ya sekta kumi na mbili (12) ambapo nchi wanachama zilianza awamu ya kwanza ya majadiliano ya ulegezaji wa masharti ya biashara ya huduma. Majadiliano hayo yanahusisha sekta sita (6) za kipaumbele ambazo ni Mawasiliano, Fedha, Utalii, Uchukuzi, Nishati na Ujenzi.

Sekta hizi zilichaguliwa kwa kuzingatia mchango wake katika maendeleo na kiwango cha mtangamano baina ya nchi

wanachama ambazo ni Tanzania, Afrika Kusini, Zambia, Lesotho, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zimbabwe, Malawi, Eswatini, Namibia, Angola, Botswana, Msumbiji, Mauritania, Ushelisheli, Comoro na Madagascar.

Vilevile, awamu ya pili inahusisha sekta sita zilizosalia ambazo ni Usambazaji, Elimu, Mazingira, Afya ya Jamii, Burudani na Utamaduni na Michezo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kutathmini kwa kina kuhusu sekta zinazoridhiwa na Itifaki hii, Kamati imejiridhisha kuwa nchi yetu iko kwenye nafasi nzuri ya kunufaika na biashara ya huduma katika sekta hizo kwenye soko la SADC ikiwa Serikali itatekeleza wajibu wake wa kuendelea kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara ya huduma nchini.

**2.3.4 Manufaa ya Itifaki kwa Nchi**

**Mheshimiwa Spika**, kulingana na mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali, kuridhia itifaki hii kutatoa fursa na manufaa yafuatayo kwa Taifa:-

a) Biashara na bidhaa zinazoendana na Huduma zinazozalishwa na kutolewa nchini zitalifikia soko la SADC lenye idadi ya watu zaidi ya milioni 360;

b) Kuongezeka kwa uwekezaji nchini, kuvutia mitaji kutoka nje (foreign capital), kukuza ushiriki wa wananchi katika kutoa huduma na kuongeza Pato la Taifa;

c) Kuongezeka kwa fursa za ajira;

d) Kuongezeka kwa ufanisi na ubora wa huduma;

e) Kuwepo kwa unafuu wa gharama za upatikanaji wa huduma katika sekta zitakazofunguliwa kutokana na ushindani;

f) Kukua kwa mitaji ya wawekezaji wa ndani kupitia ubia na wawekezaji kutoka nchi Wanachama na wale wasio wanachama; na

g) Kukua kwa teknolojia na utaalam kupitia uhaulishwaji kutoka Nchi Wanachama na wale wasio wanachama.

**Mheshimiwa Spika**, fursa hizi zinazoambatana na kuridhia itifaki zinatoa nafasi kubwa kwa Taifa letu kunufaika na Itifaki ikiwa Serikali itaendelea kuboresha mifumo itakayovutia na kuboresha mazingira Kisera, Kisheria na Kiusimamizi ya ufanyaji biashara ya huduma.

**Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kuwa kwa kuridhia itifaki hii, Tanzania sasa itakuwa katika nafasi nzuri ya kuonesha fursa zake za kibiashara ikiwa ni pamoja na kueneza utamaduni wake kwa nchi wanachama kwa kuzingatia kuwa Kiswahili kimekuwa miongoni mwa lugha kuu nne zinazotumika katika shughuli za nchi za SADC.

**2.3.5 Changamoto zinazoweza kukwamisha manufaa ya Itifaki**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi wa Kamati, imebainika kwamba zipo changamoto kadhaa zinazoweza kukwamisha ama kucheewesha nchi yetu kunufaika ipasavyo na Itifaki hii. Changamoto hizo ni pamoja na:-

i) Ukosefu wa taarifa na elimu ya kutosha kuhusu fursa za biashara ya huduma zinazopatikana miongoni mwa nchi wanachama wa SADC kwa wananchi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii) Uwepo wa Sera, Sheria na Kanuni zilizopitwa na Wakati zinazosimimia sekta ya biashara nchini;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kujadiliana na Serikali kuhusu Changamoto hizo na kukubalina kwa pamoja kwamba utatuzi wa changamoto hizi utasaidia katika kuongeza manufaa ambayo nchi yetu inaweza kuyapata kutokana na kuridhiwa kwa itifaki hii.

**SEHEMU YA TATU**

**3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wake na kukamilisha, hivyo kuwasilisha Bungeni ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba na pia kuiwezesha Serikali kuendelea na taratibu zingine za kuridhiwa kwa Itifaki hii. Aidha, Kamati inaona ipo haja kwa Serikali kuzingatia maoni na ushauri ufuatao kwa lengo la kuboresha mazingira ya utekelezaji wa Itifaki ya Biashara ya Huduma na kuleta tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

a) **Sera, Sheria na Kanuni za Biashara zilizopitwa na Wakati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inakamilisha mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni za Biashara zilizopitwa na wakati ili kuendana na mahitaji ya sasa ya biashara hasa ukuaji wa sayansi na teknolojia. Mfano wa Sera na Sheria hizo ni pamoja na Sera ya Taifa ya Uhamasishaji Uwekezaji (1996), Sera ya Taifa ya Biashara (2003) na Sheria ya Kujilinda dhidi ya Athari za Kibiashara (Trade Remedies Act, 2021), Sheria ya Uwekezaji (1997) na Sheria ya Ushindani (2003). Aidha, Serikali iboreshe mifumo ya usimamizi na uratibu wa shughuli za kibiashara ili kuleta ufanisi katika kutekeleza Biashara ya Huduma.

b) **Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi**

Kwa kuwa Sekta binafsi ina mchango mkubwa katika uwekezaji wa biashara ya huduma hapa nchini, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha Serikali inaishirikisha kikamilifu sekta binafsi katika hatua zote za utekelezaji wa Itifaki hii, ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo na uelewa wa fursa za kibiashara ili washiriki ipasavyo na kurahisisha utekelezaji wake katika kutumia fursa zilizopo;

(ii) Iweke mfumo na mkakati madhubuti wa kuhakikisha wafanyabiashara wanashiriki ipasavyo katika kuzitumia fursa zilizopo kwenye Itifaki hii na kunufaika nazo; na

(iii) Iboreshe mifumo iliyopo ya utoaji leseni za biashara ili isiwe kikwazo kwenye Biashara ya Huduma.

c) **Chombo cha Kutatua Migogoro**
**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa ufanyaji wa biashara mara nyingi huwa na migogoro inayohusisha ushuru na vikwazo visivyokuwa vya kiushuru, Kamati inashauri kwamba, ni muhimu kuanzisha chombo kitakachosimamia masuala ya kutatua migogoro ya kibiashara mara tu baada ya Itifaki kuanza kutekelezwa badala ya kusubiri hadi mgogoro utakapoibuka.

d) **Mazingira ya Ufanyaji Biashara**
**Mheshimiwa Spika**, ili Itifaki hii iweze kuleta tija inayotarajiwa kwa nchi yetu, Kamati inashauri Serikali yafuatayo: -

(i) Iendelee kuboresha na kujiimarisha katika maeneo yote yanayotumika kama kichocheo cha biashara kama vile Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia masuala ya ushindani;

(ii) Kuboresha usimamizi katika sekta zinazohusu biashara za huduma na kuimarisha miundombinu ya mawasiliano;

(iii) Kuendelea kuimarisha huduma za kimtandao Kwa kuwa dunia inakabiliwa na uhalifu wa kimtandao unaoweza kuleta tishio kubwa kwa usalama wa nchi, mashambulizi dhidi ya Serikali na kuathiri mifumo, habari nyeti na upotevu wa fedha au mapato.

Ni ushauri wa Kamati kuwa, ili kuepukana na changamoto hiyo Serikali ihakikishe kunakuwa na ulinzi wa kutosha kwenye mifumo ya kimtandao nchini; na

(iv) Kuweka mazingira mazuri yatakayovutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini na kuingiza fedha za kigeni. Kwa mfano, hivi sasa matengenezo ya meli na ndege yanafanyika nje ya nchi hali inayochangia kutumia kiasi kikubwa cha fedha za kigeni. Ni wakati sasa wa kuvutia wafanyabiashara ya huduma kuja kuwekeza kwa kujenga karakana za ndege na meli zitakazosaidia kufanya matengenezo hapa nchini.

e) **Changamoto zinazoikabili Sekta ya Usafiri**
Kwa kuwa ipo changamoto ya madereva wa malori kuzuiliwa kupita katika baadhi ya mipaka ya nchi za SADC, hali inayopelekea bidhaa kuharibika, Kamati inaiomba Serikali kuhakikisha changamoto hii inatatuliwa ili isiwe kikwazo kwenye utekelezaji wa itifaki ya Biashara ya Huduma.

f) **Mazingira ya Amani katika Utekelezaji wa Itifaki**
Kwa kuwa imewahi kutokea kwa baadhi ya nchi wanachama SADC ikiwemo Afrika ya Kusini kuanzisha vurugu dhidi ya raia wa nchi zingine ambao ni wananchi wa SADC (Zenophobia) hali iliyopelekea vifo, uharibifu wa mali na miundombinu; Kamati inashauri Serikali kuhakikisha raia wote wanalindwa ilimradi hawakiuki sheria na taratibu za nchi wanachama ili waweze kutekeleza shughuli zao kama malengo ya Itifaki hii.

g) **Kutumia Fursa za Umahiri zilizopo kwenye Itifaki (Comparative Adantage)**
**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Tanzania iko katika nafasi nzuri ya kunufaika na Itifaki hii kulinganisha na nchi zingine, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatumia vizuri uwepo wa itifaki hii katika kupeleka huduma katika nchi wananchama wa SADC, hivyo kuvutia mtaji zaidi kutoka nje. Mfano wa fursa hizo ni: -

(i) **Uwepo wa Nishati ya ziada**
Kwa kuwa ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere hadi kufikia tarehe 31 Julai, 2023 umefikia asilimia 90.19 na kwa kuwa mradi huo ukikamilika nchi itakuwa na umeme wa ziada, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali itumie fursa iliyopo katika itifaki hii ili kuuza umeme katika nchi wanachama wa SADC;

(ii) **Huduma za Afya**
Kwa kuwa huduma za afya nchini zimeendelea kuboreshwa na Tanzania imejipanga kuleta utalii wa Kitabibu, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali iweke mikakati ya kuimarisha huduma hizo ili kuvutia nchi wanachama kuja kutibiwa katika hospitali zetu, hali itakayochangia ongezeko la fedha za kigeni. Vile vile madaktari

kutoka nchini wapate fursa ya kubadilishana uzoefu na nchi wanachama wa SADC;

(iii) **Ukuzaji wa Sekta ya Utalii**
Kwa kuwa Itifaki itaruhusu uwekezaji wa hoteli za kitalii katika nchi Wanachama; na kwa kuwa nchi yetu ilishaweka viwango vya ujenzi kuanzia nyota nne na kuendelea, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha vigezo vilivyowekwa vinafuatwa badala ya kujenga kiholela na kuharibu mandhari ya maeneo yetu; na

(iv) **Uendelezaji wa Sekta ya Elimu**
Kwa kuwa Tanzania tuna wahitimu katika fani mbalimbali ikiwemo waliohitimu shahada ya Lugha ya Kiswahili; na kwa kuwa kuna fursa ya kufundisha katika nchi mbalimbali Wanachama wa SADC; Kamati inaishauri Serikali kutumia Itifaki kutangaza lugha ya Kiswahili ili kuongeza ajira kwa walimu nchini.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna mnavyotimiza majukumu yenu kwa weledi na umakini mkubwa na hivyo kuliwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ufanisi.

Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha kushughulikia azimio hili.

Kwa kuzingatia ufinyu wa muda tulionao naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb - M/Mwenyekiti
2. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb,
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb

4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb
5. Mhe Dkt. Christine Ishengoma, Mb
6. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb
7. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb
8. Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb
9. Mhe. Dkt. Medad Matogolo Kalemani, Mb
10. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb
11. Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb
12. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb
13. Mhe. Francis Isack Mtinga, Mb
14. Mhe. Lucy John Sabu, Mb
15. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb
16. Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi, Mb
17. Mhe. Eng. Samweli Xaday Hhayuma, Mb
18. Mhe. Yahya Ally Hamis, Mb
19. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb
20. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati natumia fursa hii kuwashukuru Waziri wa Viwanda na Biashara- Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri - Exaud Kigahe (Mb) na Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu- Dkt. Hashil Abdallah kwa ushirikiano wao kwa Kamati ambao umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naomba kumshukuru Mhe. David Mwakiposa Kihenzile, Mb, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati hii hadi kufikia jana tarehe 30 Agosti, 2023 kwa uongozi wake mahiri kwa kipindi chote alichokuwa kiongozi wa Kamati yetu. Aidha, tunampongeza sana na kumtakia kila heri katika utekelezaji wa majukumu yake mapya ya Naibu Waziri wa Uchukuzi.

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi (ndc) kwa kuongoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati na Bunge kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** ninaunga mkono azimio, naomba kuwasilisha.

Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb
**MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**
**31 Agosti, 2023**

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa uwasilishaji mahiri kabisa wa maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Azimio hili. Tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kupata Taarifa ya Mheshimiwa Waziri pamoja na maoni ya Kamati sasa ninayo majina ya wachangiaji na tutaanza na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud atafuatiwa na Mheshimiwa Joelson Luhaga Mpina, Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Napenda kuipongeza Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kutuletea kuridhia Itifaki hii ya *SADC*. Nawapongeza wote wa hapo Wizarani kwa juhudi zao mbalimbali za kuhakikisha nchi yetu inakwenda kunufaika na fursa mbalimbali zilizopo katika *SADC* na sehemu nyingine katika dunia yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mapendekezo ya Kamati kwa kuishauri Serikali. Kati ya nchi tano ambazo hazijaridhia Azimio hili na Tanzania imo, leo hii tunakwenda kuridhia Azimio hili kwa manufaa ya nchi yetu, manufaa ya Watanzania na manufaa ya wafanyabiashara wetu wanaotoa huduma mbalimbali katika nchi. Tutanufaika na fursa mbalimbali zikiwemo biashara za huduma kama vile elimu, afya, usafirishaji na mambo mengine yanayohusu kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa hapa suala la kwamba tutapata fursa ya kukitumia na kukieneza Kiswahili katika ukanda huu wa *SADC*. Ushauri wangu kwa Serikali, tuitumie vema

fursa hii ya uwekezeaji kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania na vijana wetu ambao tayari ni weledi wa Lugha ya Kiswahili. Tuhakikishe Tanzania tunaendelea kukihakikisha Kiswahili ni cha Tanzania kuepusha soko hili likatekwa na nchi nyingine wakajifanya wao ndiyo wakuu wa Kiswahili. Nashauri tuendelee kuhamasisha vijana wetu kutumia fursa hii ya ajira kwa soko la kueneza Kiswahili kwa fani mbalimbali ualimu, ukalimani, uhadhiri na mambo mengine ya kuandika vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakwenda kunufaika pia na fursa nyingine kwa upande wa mazingira, tutanufaika pia kwa fursa za watoa huduma ikiwemo mawasiliano elimu na afya. Naishauri Serikali tuweke mazingira mazuri kwa watoa huduma wetu tulionao na Serikali kuanzisha kitengo maalum ndani ya Wizara cha kuibua fursa ambazo watakwenda kuwekeza katika hizo nchi nyingine za *SADC*. Kwa sababu, isiwe wao wanakuja kwetu tu kutumia fursa zetu lakini sisi hatupati kwenda. Ni vyema sasa tukawasaidia wafanyabiashara wetu hawa wa huduma namna ya fursa zilizokuwemo kwenye nchi za wenzetu za *SADC* ili tuwe tunabadilishana uzoefu na maarifa wao wanakuja na sisi tunakwenda. Tukifanya hivyo na sisi tutajitangaza zaidi kwa fursa mbalimbali za uwekezaji katika nchi nyingine za *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusaidie kuwawezesha kimitaji wafanyabiashara wetu watoa huduma, kwa sababu bado kuna hili tatizo la mitaji ya kutosha. Tuwasaidie namna ya kupata mitaji katika benki ili na wao waingie kwenye huu ushindani kwenye kuwekeza katika nchi mbalimbali za *SADC* ili tupate hayo manufaa na sisi ya kuingia kwenye *SADC*. Tukifanya hivyo wafanyabiashara wetu watoa huduma watakuwa na wao na ujasiri watakuwa na uelewa na weledi wa kuwekeza na watatoka uoga kwa sababu wakati mwingine ni hofu tu lakini tukiwatoa hofu tukawapa elimu na tukawapa maarifa ya kuingia, wataweza kuingia kwenye ushindani huu wa soko la kutoa huduma mbalimbali katika nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Bunge likubali kuridhia Azimio hili ili tuendane na wakati tusiwe tumeachwa nyuma twende sambamba na hali ya mabadiliko ya dunia ya sasa ili

kuibua fursa za uwekezaji kwa wananchi wa Tanzania fursa za ajira, fursa za masomo na fursa nyingine za kuinua uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija tunakushukuru. Mheshimiwa Joelson Luhaga Mpina atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Mohamed Issa ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa niweze kuchangia kuhusu hii Itifaki ya Biashara ya Huduma ya *SADC*. Awali ya yote niwapongeze sana Wabunge wenzetu na baadhi ya Mawaziri ambao wameteuliwa na wengine wamebadilishiwa nafasi zao. Tunawatakia kila la kheri wakati wa kula kiapo chao ili waje hapa Bungeni tufanye kazi za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia soko la *SADC* tunazungumzia soko ambalo nchi yetu inauza bidhaa na huduma takriban zaidi ya shilingi trilioni 4.5 kwa mwaka. Kwa mfano, mwaka 2022, mauzo yetu katika nchi za *SADC* tumeuza zaidi ya shilingi trilioni 4.5. Kwa hiyo, unapoliendea soko la *SADC* unaliendea soko ambalo ni kubwa, soko ambalo tunalitegemea na ni soko ambalo ni la pili kwa ukubwa katika masoko ambayo tunayauzia bidhaa zetu ikitanguliwa na Asia na masoko mengine kama la *East Africa*, *Europe*, *AGOA* na masoko mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, soko la *SADC* ni soko kubwa ambalo tunapofikiria kufanya jambo lolote ni lazima tulifikirie kwa umakini mkubwa na tuhakikishe kwamba tuko vizuri. Tunapozungumzia hii Itifaki ya Biashara ya Huduma *(Protocol on Trade in Service, 2012),* kabla hatujakubaliana kuridhia ni lazima tupewe majawabu kwenye mambo fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni lazima tujiulize kwa nini Azimio hili tangu lisainiwe na Wakuu wa nchi mwaka 2012, leo ni

miaka 11 halijawahi kuridhiwa? Sababu zilizosababisha lisiridhiwe kwa miaka yote hiyo 11 ni nini? Mazingira gani yalikuwepo, Azimio hili linazaliwa tarehe 18/08/2012, sasa mpaka leo miaka 11 ndiyo linaletwa hapa Bungeni, kwa nini? Kwa nini halikuletwa kabla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua Dkt. Stergomena Lawrence Tax ambaye anatoka Tanzania ndiye aliyekuwa Katibu Mtendaji wa *SADC* toka mwaka 2013 mpaka 2022 na leo ni mwaka 2023. Wakati akiwa kule Azimio hili halikuwahi kuletwa Bungeni wala halikuwahi kuidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais mstaafu wa Tanzania ambaye alisaini hii Itifaki mwaka 2012, amekaa madarakani miaka minne zaidi mpaka mwaka 2015, lakini hakuwahi kuleta hili Azimio ndani ya Bunge liridhiwe. Aliyelisaini hakuwahi kulileta hapa Bungeni liridhiwe, leo kwa nini linaletwa? Sababu za kuchelewa muda wote huo ni nini? Kama kulikuwa na kasoro za kurekebishwa mbona hatujaambiwa kama zimerekebishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaletewa hili Azimio kuridhia lakini tuna *SADC Protocol for Finance and Investment,* tuna *SADC Protocol on Trade,* hizi protokali zote zipo. Hii *protocal* tunayotaka kuiridhia leo inaenda kutibu nini? Inaenda kuziba changamoto gani ambayo haipo katika *protocol* au katika Itifaki ambazo tumeshaziridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ile Ibara ya 16(2) imezungumzia kwamba tunataka huduma ya biashara kwenye hizi sekta sita. Je, tunaenda kunufaika katika muktadha gani? Tunaenda kufanyaje, kwa mfano kwenye TEHAMA tunaenda kufanya nini na TEHAMA? Kwenye ujenzi tunaenda kufanya nini na ujenzi? Haijaelezwa kwa kina. Ukisoma taarifa ya Waziri mwenyewe anayewasilisha Itifaki hii, hata taarifa ya Kamati yenyewe huoni ni kwa muktadha gani na kwa namna gani tunakwenda kufanya hizi biashara ambazo sasa hivi tunashindwa kuzifanya kwa sababu hii Itifaki haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haijaelezwa nchi tano ambazo mpaka sasa hivi hazijaridhia hili Azimio. Haijaelezwa kwa nini nchi tano kwa muda wa miaka 11 hazijaridhia hili Azimio. Lazima kuna tatizo, kwa nini halisemwi? Kama kulikuwa na tatizo na tuliliona kwamba ni tatizo, tumefanya marekebisho gani na kwa nini leo tunataka Bunge hili lishiriki kuridhia hili Azimio bila kuelezwa matatizo yaliyopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 6(4) inazungumzia suala la *CMT, Committee of Ministers Responsible for Trade,* kuanzisha utaratibu wa kinidhamu. Mawaziri wanaoshughulika na viwanda na biashara wanapewa mamlaka ya kuweka utaratibu wa kinidhamu huku tukijua chini ya *WTO* utaratibu wa kinidhamu wa kibiashara wa pamoja umeshawekwa katika *General Agreements on Trade and Service (GATS)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu ulishawekwa, sasa hii *duplication* ya kuweka utaratibu mwingine inatoka wapi? Kama Mawaziri wakiruhusiwa wakaenda kutengeneza mkanganyiko, hatuoni kwamba tunaweza kusababisha Nchi za *SADC* kuwa kwenye migogoro muda wote, kusuluhisha matatizo kila leo? Kwa nini tusitumie zile *general rules,* zile *general disciplines* zilizowekwa kwenye *GATS* badala ya hao Mawaziri kupewa fursa ya kwenda kuandaa na kutengeneza utaratibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 8(2) imeweka sharti la mabadiliko yote ya sheria, kanuni na miongozo inayoathiri biashara ya huduma ya Nchi Wanachama kupeleka taarifa *TNF Services* yaani *Trade Negotiation Forum Services.* Takwa hili linaweza kutuletea matatizo makubwa, tunapotunga sheria zetu hasa zile *domestic physical legislations* ambazo katika nchi yetu hazitabiriki, mara nyingi tumekuwa tukianzisha tozo, faini, ada na ushuru mpya kila mwaka. Unaanzisha baadaye unafuta, baadaye unapunguza, baadaye unaondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukifanya hivyo kila Mwaka wa Fedha ukifika, tunabadilisha sheria, tunaongeza tozo hii, tunapunguza tozo hii, tunasamehe ipi? Haya yote yamekuwa yanafanyika bila utafiti wowote na bila tathmini yoyote. Sasa

kama kila mwaka tunaripoti kwa nchi zetu wanachama ambazo tunategemea soko kubwa sana kutoka kule SADC, tukiwa tunafanya hayo marekebisho kila mwaka, tunaweza kutengeneza mkanganyiko mkubwa sana na nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 16(2), tunaposema tunaenda kuingia kwenye huduma katika maeneo ya mawasiliano, fedha, ujenzi na usafirishaji tumejiandaaje ndani ya nchi? Mbona miradi mingi tuliyonayo sasa hivi hatuwapi wenzetu wa *SADC*? Hata miradi ambayo inaweza ikatekelezwa na wenzetu wa *SADC* mbona hatuwapi? Miradi ya TEHAMA mingapi tumeingia hapa na mikataba ya nchi za nje? Kwa mfano, Mradi wa *CISCA* ambao tungeweza kuutekeleza ndani ya Nchi zetu za *SADC*, Mradi wa TEHEMA wa *TANESCO* unatekelezwa na *Mahindra* T*ech* kazi ambayo ingeweza kufanywa na vijana wetu wa *e-GA* waka-*develop* huo mfumo, lakini tumewapa watu wa nje ya ukanda wa *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo tunapozungumza, tunaji-*limit* kabisa, tunaandika hapa, tunaruhusu mpaka kanuni za nidhamu ziwekwe. Mpaka tunaenda kuweka namna ya utatuzi wa migogoro kwa maana ya ile *Annex one* iliyowekwa katika Itifaki hii. Hivi tuna maandalizi gani wakati hata shughuli tulizonazo hivi sasa zote tunawapa watu wa nje ya ukanda? Tunafanya hivi kumfurahisha nani? Mbona hata maandalizi ya ndani ya kuridhia Itifaki hii hayapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye ujenzi na uchukuzi, hata barabara fupi tu, za hela ndogo *consultant* anatoka Ulaya, *consultant* anatoka Asia. Hata kwa mambo ambayo tungeyafanya sisi ndani ya ukanda. Leo tunajifurahisha nini kusema kwamba tunaingia mkataba huu wakati hata miradi ambayo naizungumza tumefunga mikataba nje ya ukanda, wakati Itifaki hii Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alisaini toka mwaka 2012, kuna marekebisho gani toka kusainiwa kwa Itifaki hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia ushirikiano wa fedha wa sekta ya fedha. Sekta ya fedha nchini hapa na hata

*SADC* wote tunategemea Dola. Sasa hivi Dola hakuna, Dola zimeadimika, wafanyabiashara hawapati Dola, hivyo hawawezi kuagiza mizigo, tunafanyaje? Maelezo yanayotolewa na Serikali, uwekezaji umeongezeka ndani ya nchi maradufu, watalii wameongezeka nchini maradufu, Dola zimeenda wapi kama uwekezaji, utalii na mauzo ya nje yameongezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti,…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Luhaga Mpina, malizia sentensi moja ya mwisho.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha kwa kusema kwamba, Serikali ni lazima itatue tatizo la kuadimika kwa dola na hasa ninavyoona sababu ambayo haizungumzwi ni suala la ufisadi mkubwa ulioripotiwa na *FIU* kwa kuonyesha miamala shuku ya zaidi ya shilingi trilioni 280. Inawekana dola zetu zimetoroshwa kupitia mipakani na kwenye benki na leo nchi haina dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa maelezo haya niliyoyatoa ambayo sikuweza kuyasema yote, nasema kwamba siwezi kuridhia Azimio hili na nalishauri Bunge kwamba lisiridhie hii Itifaki kwanza *unless* tupate maelezo ya kina ya Waziri nini kilichosababisha miaka 11 Itifaki hii haikuridhiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Luhaga Mpina. Mheshimiwa Rashid Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Issa na Mheshimiwa Samwel Hhayuma jiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika Azimio hili ambalo liko mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza sana Waziri mwenye dhamana ya Viwanda na Biashara kwa kuleta Itifaki hii. Kipekee nawapongeza Kamati kwa namna

ambavyo wamechakata na kutoa maoni ambayo na sisi tunaweza kupata mwanga wa kuweza kushauri katika kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ya Mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasi kidogo kwa nini Itifaki hii imechelewa, lakini sio jambo geni kwa Tanzania, mara nyingi mambo mengi huwa tunachelewa, ila sasa kwa sababu sasa hivi dunia inakwenda kasi, ni vizuri tukipata fursa nzuri kama hizi, tukajitahidi kwenda nazo kwa haraka zaidi. Ninachotaka kusema ni kwamba sisi kabla ya mwaka 2000 Sera yetu ya Mambo ya Nje ilikuwa ni ukombozi wa Bara la Afrika na tulijikita zaidi Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu nchi zote hizi ambazo tunazozizungumzia, ukiacha zile ambazo zimepata uhuru kabla yetu au karibu na sisi, nyingine zote tumeshiriki kwa jasho na damu kusaidia kuzikomboa. Jambo hili lilikuwa na maana sana kwamba baada ya ukombozi ule wa kupata uhuru, basi wakishakuwa huru ni lazima tutengeneze utengemano kama huu wa kufanya biashara, kwa hiyo kwa hatua hiyo naipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningetaka niliseme ni kwamba, Sera yetu ya Mambo ya Nje wakati huo ilikuwa ni ya ukombozi, kwa hiyo ni vizuri tukaipitia upya Sera yetu ya Mambo ya Nje ya sasa ya *Economic Diplomacy* yaani Diplomasia ya Uchumi kwa sababu bado kuna maeneo mengi ya kiuchumi ambayo hatujayatumia vizuri kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi nchi tunazozizungumzia hapa ukiacha nchi mbili kwa maana ya Afrika Kusini na Angola, hizi nyingine zote *GDP per capita* tunawazidi, kwa maana sisi uchumi wetu uko juu zaidi. Sasa kwa jiografia ilivyo na utamaduni ulivyo ni kwamba nchi hizi karibu sehemu kubwa hata kabla ya kuridhia hii Itifaki tunazihudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mambo ambayo yametajwa kwenye Itifaki kwa mfano huduma za kifedha, zipo nchi kama DR Congo tayari kuna huduma za kifedha kwenye hizo

nchi, kwa maana mikataba ya nchi na nchi, tayari kuna Benki ya *CRDB* ina-*operate* pale Lubumbashi. Ukienda Comoro tayari kuna Benki ya *Exim* nadhani na *CRDB* pia wana-*operate* pale Comoro. Kwa hiyo, utaona kwamba zile *bilateral treaties* tayari zinafanya kazi nje ya Itifaki hii kwa maana ya nchi na nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija katika mawanda mazima ya mawasiliano, kwenye mawasiliano tunazungumzia suala zima la uchukuzi na suala zima la *logistics*. Hii inafanyika, hata kwa kampuni moja moja lakini pia kwa nchi kwa maana kwamba tunaposafirisha bidhaa kutoka katika bandari zetu kwenda katika Nchi hizi za *SADC* bado kuna eneo ambalo tayari tunafanya. Kwa hiyo Itifaki hii iende ikaboreshe na kutengeneza mnyororo mzima wa kuthaminisha Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo hatukufanya vizuri na ambalo tunataka Itifaki hii ambayo tunairidhia baada ya miaka 11, twende tukaisimamie ni suala zima la elimu. Kama ambavyo nimetangulia kusema kwenye utangulizi ni kwamba kwa kuwa tumeshiriki katika ukombozi wa hizi nchi maana yake tumezisaidia kwa namna moja ama nyingine hasa katika eneo la ulinzi na usalama *(peace keeping)*. Ukifika huko mara nyingi askari polisi na jeshi kwa ujumla wake wamepewa mafunzo na Watanzania na ndiyo maana ukifika kwenye nchi hizo ukikutana na maaskari wanajua vizuri hata Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la elimu tunatakiwa tuingie hapo kupeleka huduma. Kwa mfano, huduma za elimu ya uhandisi, bado tuna wahandisi wengi hapa ndani ya nchi na hakuna ajira, ni lazima tutengeneze mkakati wa kuhakikisha tunasukuma watu wetu wa kada hiyo kwenda kufanya kazi katika nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la afya, Wahadhiri wa vyuo tunatakiwa tuwapeleke huko kwa sababu sisi tuna idadi kubwa na wenzetu hawa baadhi ya nchi bado hazijajitosheleza, ni lazima tutumie fursa hiyo kupeleka watu wetu kutoa huduma hiyo ya elimu katika hizi nchi. Kwa sababu za kidiplomasia nashindwa kuzitaja, lakini tumefanya utafiti wa kina zipo nchi

bado zinahitaji huduma ya Madaktari, zipo nchi zinazohitaji huduma ya Wahandisi na zipo nchi zinahitaji huduma ya Manesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo Watanzania wamethubutu wenyewe kwenda kwenye hizo nchi, lakini Tanzania haiwatambui, kwa maana Balozi zetu zilizopo kule haziwatambui kwa sababu wameenda wenyewe. Kwa hiyo, tunachotaka kumshauri Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, aitumie vizuri Wizara ya Mambo ya Nje tuhakikishe kwamba Mabalozi wetu kwenye diplomasia ya uchumi kwa Nchi za *SADC* tuna-*capitalize* kwenye hili eneo la kuweza kusaidia Watanzania ambao wamesoma na ndani ya nchi tumeshindwa kuwaajiri, lakini kuna fursa hiyo nje ya Tanzania, basi waipate kupitia eneo hili la *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo liko kwenye Ibara ya 16 ni suala zima la afya. Afya hapa imetajwa kwa ujumla na nimeshataja katika maeneo hayo ya kitaaluma, lakini kwenye *logistic chain* ya usambazaji wa madawa, hapa nataka niweke wazi kwamba hata *MSD* waliwahi kupata zabuni ya kusambaza dawa katika nchi zote za *SADC* wakati huo zikiwa 13 na sasa zimefika 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana kwamba tunaweza tukahakikisha pia tunaishirikisha vema Wizara ya Afya kupitia *MSD* kwenda kutumia fursa hiyo ya kusambaza madawa katika hizo nchi. Imeonekana kwamba usambazaji wa dawa unaofanywa na *MSD* ndani ya Tanzania ni usambazaji wa kiwango cha kimataifa, hivyo wenzetu hawa wamevutiwa. Kwa hiyo, tutumie fursa hiyo ya kwenda kutengeneza *logistic* ya kwenda kusambaza dawa katika *SADC,* lakini wakati huo huo tukiitumia kama *advantage* ya kuhakikisha kwamba tunafungua viwanda vingi vya madawa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dawa nyingi ambazo tunazisambaza katika nchi yetu hazizalishwi Tanzania. *Source* kubwa ya madawa yetu yanatoka Ujerumani na India. Kwa hiyo, maana yake kama *SADC* watamchukua *MSD* kwenda kusambaza madawa katika nchi zao inawezakana kabisa kwamba na dawa ambazo zitapita Tanzania au zitazalishwa

Tanzania soko letu litakuwa kubwa zaidi. Tukiwekeza katika viwanda vya madawa maana yake dawa zetu zitakuwa ni sehemu ya kwenda kusambazwa katika Nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningetaka kushauri ni suala zima la ukuzaji wa Lugha ya Kiswahili. Hapa napo ni lazima tuwe na mkakati madhubuti. Kiswahili hiki tunachozungumza leo sio cha kwenda kufundishia. Ni lazima tujipange upya, BAKITA na Wizara inayohusika tuanze kuandaa wataalam, *Linguists* ambao watakwenda kufundisha hicho Kiswahili katika nchi ambazo tunakusudia. Haitawezekana kumfundisha Kiswahili kama hujui lugha yake. Zipo nchi zinazungumza Kireno, zipo nchi zinazungumza Kifaransa na zipo nchi zinazungumza Kiingereza. Kwa hiyo, ni lazima tuwaandae watu wetu watakaokwenda kufundisha Kiswahili wawe wanazijua hizo lugha ili waweze kurahisisha uwasilishaji na mawasiliano kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini sio kwa umuhimu nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, lakini tunataka kuona mabadiliko makubwa katika eneo hili la *SADC* kwa sababu kwa jiografia ya nchi yetu ndiyo eneo kubwa zaidi ambalo linaingiza pato kubwa baada ya India. Sehemu nyingine ambayo tuna soko kubwa la watu hawa zaidi ya milioni 360 ni ukanda wa *SADC*. Kwa bahati nzuri ni kwamba ukanda huu unatutegemea zaidi sisi, kwa hiyo sisi katika Itifaki hii maana yake tunakwenda kupiga *comparative advantage* ya uwepo wetu katika *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, nakushukuru sana kwa nafasi, naunga mkono Itifaki hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, ahsante sana. Mheshimiwa Mohamed Issa atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma, Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala jiandae.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kutoa mchango wangu katika mjadala uliopo hapa ama Azimio lililoletwa na

Serikali. Pia napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijalia afya nikaweza kusimama kwenye Bunge letu hili kuchangia Azimio hili ambalo limeletwa kwetu leo ili kuweza kuleta mustakabali wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio lililopo leo ni *Protocol of Trade in Service*. *Protocol* hii ni kwa ajili ya nchi za Kusini mwa Afrika kuweza kushirikiana katika biashara ya huduma katika nchi hizi ambazo ni wanachama. Itifaki hii inalenga kuondoa vikwazo na masharti ya taratibu za huduma ya biashara katika nchi wanachama. Kwanza ningependa kuipongeza Serikali kwa kuleta Azimio hili kwa sababu linakuja kuleta maendeleo chanya kwa wananchi wetu ambao wanatoka katika Jumuiya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mategemeo yetu Azimio hili litakuja kuisaidia nchi yetu baada ya kuridhiwa. Kwa nini nasema hivyo? Watanzania tumekuwa tukifanya biashara hizi kabla ya kuridhiwa Azimio hili, lakini tumekuwa tukifanya biashara kwa mashaka na vikwazo vingi bila kuweza kupata njia ya kutatua vile vikwazo, sasa muarobaini wa matatizo ya wafanyabiashara ya huduma unakuja kupatikana. Biashara hizi za huduma kama vile elimu, *transport* na mambo mengine, nchi yetu imekuwa ikipata changamoto nyingi, kwa hiyo sasa tukiridhia Azimio hili, changamoto hizi zitakuja kuondoka. Napenda kushauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukipata changamoto tukitumia zile *certificates* za Jumuiya hii bila ya kupata huduma stahiki kwa sababu tulikuwa hatujaridhia Azimio hili. Azimio hili wenzetu nchi wanachama walianza kuridhia mwaka 2022 ingawa lilisainiwa mwaka 2012. Kiukweli hatujachelewa kuridhia Azimio hili, ni kwamba tupo katika wakati mzuri na si vizuri katika jambo ukawa mtu wa kwanza ni bora kuchunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kuchelewa kulileta Azimio hili kwa sababu ni lazima tuangalie kwamba wale wenzetu walioingia wamekutana na changamoto gani ili na sisi tuweze kujifunza kupitia kwao. Kwa hili, naipongeza Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye hoja ambazo nahisi zinahitaji kurekebishwa. Nchi yetu ya Tanzania imeingia mikataba mingine na nchi ambazo si wanachama wa Jumuiya hizi. Napenda Wizara yetu au Serikali yetu ikaliangalia hili tusije tukaathiri ile mikataba ambayo tumeingia na nchi nyingine tukashindwa kufanya nao biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napendekeza nchi yetu ijikite kwenye kutoa hizi *National ID* na siyo nchi yetu tu, nchi wanachama zote ili kusiwe na mgongano kwa raia ambao hawahusiki ndani ya nchi hizi wanachama ama wakaenda kutoa huduma wakasema kwamba wanatoka katika nchi wanachama. Kama vile watu wanaoongea Kiswahili sana katika nchi ambazo siyo wanachama, wakaenda nchi nyingine wakasema wanatokea Tanzania. Kwa hivyo, suala la *National ID* ni muhimu sana ili liweze ku-*facilitate* mambo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kama lilivyosemwa na Kamati yetu hapa, kuhusu Sera na Sheria zilizopitwa na wakati. Ni muhimu sana hili tuweze kulipitia, tukazitengeneza ili wananchi wetu wasiwe wana vikwazo kuingia kwenye soko hili la Jumuiya hii ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo jema. Tufanye haraka turekebishe sheria ambazo zimepitwa na wakati ili wananchi wetu waweze kuingia kwenye soko hili vizuri. Nchi yetu itoe elimu kwa wananchi wote kulifahamu Azimio hili ili waweze kuchangamkia fursa ambazo zipo katika katika hili Azimio. Hilo ni jambo kubwa sana kwa sababu wananchi wakati mwingine kama hawana uelewa, basi inaweza ikawa fursa hizi zikatumiwa na watu wengine kuja hapa kuwekeza wakati sisi tuna uwezo wa kwenda kuwekeza katika nchi ambazo tumeridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilalopenda kuchangia ni suala la leseni za biashara. Leseni za biashara ziweze kutolewa katika masharti ambayo ni nafuu na kwa haraka na ikiwezekana kusiwe na mlolongo wa leseni. Leseni ya biashara iwe moja ili kuweza ku-*facilitate* kwa haraka ufanyaji wa biashara wa wananchi wetu katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingi ambazo wananchi wetu wanakuwa wanazipata. Mfano, madereva wanavyokwenda nchi nyingine, wanakwama mipakani kwa sababu ya *logistics* nyingi ambazo zinafanyika pale, ukitoka Tanzania kuingia *border* nyingine. Napendekeza suala hili lifanywe kwa haraka, ianzishwe *one stop center* kwa nchi hizi za Jumuiya ili watu wanapokwenda au wafanyabiashara hawa wa ma-*truck* au wasafiri, wasikutane na changamoto hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakaribia mwisho wa mchango wangu, kuhusu suala la usimamizi wa sheria. Usimamizi wa sheria zetu inakuwa ni changamoto, kwa hiyo, hili napendekeza kwamba Serikali iwe makini katika usimamizi wa sheria ili kuona kwamba hii fursa haitumiwi na watu ambao siyo wanachama. Azimio hili linakuja lakini pia nchi mwananchama itazingatia sheria zake ilizojiwekea. Siyo kwamba watu wataingia tu kiholela kwa vile tupo kwenye Azimio, napendekeza nchi yetu, watendaji wasimamie sheria tulizoziweka ili kuepuka kupoteza haki zetu kwa sababu katika nchi yetu, nataka nitoe mfano. Mfano ni upande wa Zanzibar, mtu mgeni haruhusiwi kumiliki ardhi lakini sasa hivi ukienda Zanzibar, ukifanya utafiti, basi utakuta asilimia 25 – 30 ni wageni wanamiliki ardhi bila kufuata sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ndilo nchi tunakwama kwa hiyo tunatakiwa tusimamie zile sheria zetu tunazojiwekea na kama hazifai basi tuziondoe, kama tunavyoshauri kwamba sheria zilizopitwa na wakati. Kwa sheria ambayo tunaona ina maslahi, isimamiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nataka kuchangia suala la lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili *original* ni Tanzania. Lugha hii kwa nini isiwe ni moja ya tunu yetu? na kwa nini tusiisimamie dunia ikajua kwamba *original* ya lugha ya Kiswahili ni Tanzania. Hili, kwa sababu tumeridhia vitu kama hivi, kuna soko la Afrika pia linakuja, kwa nini tusijidadavue kuona kwamba lugha ya Kiswahili *original* yake ni hapa ili kuweza kutengeneza *icon* ya nchi yetu kwamba lugha ya Kiswahili inatoka hapa na tukaweza kupata mambo mengi ya ndani ya Azimio letu hili na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge liridhie Azimio hili. Ahsante, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Issa, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Samweli Hhayuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu wajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Itifaki hii ya biashara ya huduma ya *SADC*. Kabla ya kuanza mchango wangu, niungane na baadhi ya Wabunge ambao wamepongeza Wabunge wenzetu ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais kwa nafasi mbalimbali ili kumsaidia kazi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na timu yake nzima akiwemo Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi wanavyofanya kazi nzuri ya kuwaunganisha wafanyabiashara wetu. Nimeona mara nyingi akikutana na wafanyabiashara ili kuwaonesha fursa zilizopo na namna ambavyo wanaweza kushirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmoja kati ya ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais ni aliyekuwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile. Ninampongeza sana kwa sababu Mheshimiwa Rais amemuamini. Mwenyekiti wewe ni shahidi, Makamu Mwenyekiti alipowasilisha wasilisho na maoni ya Kamati aliwasilisha vizuri sana na mimi nachukua nafasi hii kumpongeza, ametuwakilisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nachangia maeneo machache. Itifaki hii ikiridhiwa, soko la huduma litaongezeka kutoka hii ya kwetu ya shilingi milioni 61 kwenda shillingi milioni 360. Hili ni ongezeko kubwa na nasema tu kama Mheshimiwa Shangazi alivyotangulia kusema, sisi kwenye Kamati, tumeichakata, tumeangalia na tumeona kwamba kwa kweli ni fursa ambayo tumechelewa kuichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba Tanzania siyo wadhaifu tunapongia kwenye mjumuiko huu wa soko letu kutanuka. Mheshimiwa Shangazi amejaribu kueleza fursa ambayo tunayo na *GDP* yetu ni kubwa kwa maana ya watu ambao tunaweza kuwa na mashaka nao labda ni Afrika Kusini. Pia ukiangalia kwenye sekta ya huduma naona tupo nafasi nzuri zaidi. Nawashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba hii Itifaki tuiridhie na muhimu sana tujiandae vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya sekta ambayo tunaiangalia ni sekta ya ujenzi. Kwenye sekta hii ya ujenzi fursa zilizopo ndani ya nchi bado tunazitoa kwa wageni. Fursa itaongezeka maana yake yawezekana sisi Watanzania tusinufaike sana. Naiomba Serikali kwenye eneo hili tujaribu kuangalia namna ambavyo tunaweza kuwawezesha wataalam wetu wa ujenzi, makampuni ya ujenzi ili tuweze kupata fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa iliyopo kwa watu wetu ni mitaji. Kingine ambacho kipo ni namna ambavyo makampuni ya kizawa yanahudumiwa ukilinganisha na wageni. Ukiangalia kwenye *tendering process* watu wetu wataambiwa kwamba wafanye kazi wa-*rise certificate* ndiyo wanapata malipo, wakati mwingine malipo hayaendi kwa wakati, kwa mantiki hiyo tuna-*drain* uchumi wao na tunawachelewesha watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitanua soko hili tuweze kunufaika, lazima tutengeneze *mechanism* ya kuwasaidia Watanzania kwanza kukamata soko hili la ndani pia kukamata soko hili tunalolitanua la nchi za Kusini mwa Afrika – *SADC*. Ukienda kwenye benki zetu, mtu ana mkataba wa kufanya kazi hata na Serikali ya Tanzania, mlolongo ni mrefu sana, utaratibu wa kupata mkopo ni mgumu, namna ya kuwawezesha lazima itafutwe ambayo ni rahisi ili hili soko tunalolitanua tunufaike nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye sekta ya fedha kutafuta mikopo, ajenda ya kwanza watakwambia kwamba watakuwa na *valuer* wao kama wewe una mali ambazo

hazihamishiki, wa benki yenyewe. *Valuers* ninavyohamu huwa wanasajiliwa, *valuer* ambaye utapewa na benki atafanya *assessment* ya *collateral*, baada ya kufanya *assessment* atakuja na maneno mengi, mtaenda *back and forth* isiyopungua miezi minne mpaka na kuendelea. Tukienda na mwendo huu kwenye soko hili ambalo tunafungua, pamoja na *strengths* tulizonazo, hatutawasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kazi yako ni kushamirisha biashara. Kazi kubwa uliyonayo mbele yako ni kukamata hili soko la watu miliono 360, ili tuweze kunufaika kwenye eneo hilo, kaa na Waziri wa Fedha ili kwenye sekta hii ya fedha, vikwazo ambavyo wanapata Watanzania viweze kuondolewa ili tuweze kunufaika na isije ikaonekana kwamba tumepata fursa lakini bado hatuna nafasi ya kuikamata.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye eneo la taarifa na Watanzania kujua fursa zilizopo. Kwenye eneo hili Mheshimiwa Waziri lazima ufanye kazi ya ziada, tembea na Watanzania, itazame Tanzania, angalia hali zao, kama unavyokuwa na mahitaji muhimu kwenye pochi yako, panga na hitaji la Watanzania, Serikali imuwezeshe Waziri wa Viwanda na Biashara kuwa na fedha za kufanya hamasa kwa Watanzania, kuwa na namna ya kuyafikia hayo masoko, kufanya maonesho maeneo mbalimbali kwa yale mazuri sisi tuliyonayo ili hatimaye hili soko tuweze kuliteka. Ni fursa kwetu, lazima tuchangamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda na utendaji ule wa kawaida wa Kiserikali, haitatusaidia na tutakwama. Fursa iliyojitokeza lazima tuikamate, ni kweli tumechelewa. Ninachoomba tu, Serikali kwa maana hasa Wizara ya Viwanda na Biashara, jitoe kwenye ule mfumo wa kawaida wa urasimu wa Kiserikaliserikali. Jiweke kama wewe ni sehemu ya sekta binafsi, tembea na sekta binafsi kila sehemu ili hatimaye Watanzania tuweze kunufaika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania kwa sasa ukiangalia malalamiko mengi ambayo watu wetu wanayo si makubwa

kwenye soko hili la Afrika Mashariki. Moja limeshasemwa kwamba kwenye mipaka ile zile *blocks* za kuwazuia watu, mfano madereva wa *trucks*, malalamiko yalikuwa ni mengi. Ninaamini kwa Itifaki hii tukishairidhia, yale malalamiko yote yataondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati tumeona eneo hilo la sera zetu, sheria zetu, kanuni zetu za biashara lazima ziweze kufungua fursa tukimbie, tusitanguliwe na wenzetu. Lingine, kwa sababu Bunge hili ni chombo cha wananchi, niwaombe Watanzania wenzangu hii ni fursa tukimbizane nayo, tuwahi, tukichelewa tutakuta mwana si wa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tunapaswa tulirekebishe kabla hatujaenda mbali sana ni eneo la kodi. Kwa mfano, kwenye malori kwa sababu eneo la usafirishaji ni sehemu ya huduma, sisi Watanzania, mtu akishakuwa na lori mbili anaanza kulipia *VAT*, gharama zipo nyingi na kila lori ina *EFD machine*. Sasa tuangalie kama hizi changamoto ambazo tunazo na watu wa malori mara nyingi wamekuwa wakilalamika. Kama kwetu ipo, je, kwa wenzetu ipo hivyohivyo? Kwa sasa ukitembea barabarani utaona lori nyingi sana ambazo zimesajiliwa nchi jirani ndiyo zinazosafirisha mizigo kutoka bandarini kwetu zinaenda nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hii changamoto, na wapo Watanzania ambao wameshasajili. Mtu ana lori kumi, lazima atafute jina la mtoto wake, ana Watoto wangapi, akasajili kwa marafiki ili angalau kuweza kumudu gharama. Wanalalamika sana gharama za uendeshaji, kodi ni kubwa. Tuangalie hizi changamoto na maeneo mengine, tukiweza kuyatibu na tukachangamkia, ninaamini fursa hii ni nzuri na itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, niliona nichangie eneo hilo. Nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mhandisi Samweli Hhayuma. Nilimtaja Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, atafatiwa na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipatia wasaa ili niweze kutoa mchango wangu kwa Azimio hili. Nitambue pongezi zilizotolewa na Wabunge wenzangu pamoja na Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu. Kwa hiyo, nami niunge mkono tu pongezi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili lina mawanda mapana na linatuonesha dira kama Taifa na manufaa mapana na makubwa ndani ya Taifa letu. Pamoja na hayo manufaa makubwa yanayoonekana kwenye hili Azimio, kuna mambo kadhaa ambayo kama nchi, kama Serikali lazima wayaangalie kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaomba kuyasema machache. La kwanza ni suala zima la biashara zetu za ndani kwanza. Leo biashara ndani ya nchi, bado kuna purukushani nyingi sana kuhusiana na suala zima la sheria, kodi na mambo kadha wa kadha. Sasa tunapokwenda kujiunga kwenye jumuiya hii ni lazima tuone: Je, hivi sisi kama nchi, changamoto zetu ndani ya nchi kwa wafanyabiashara wetu tumezitatua kwa namna gani? ili tunapotoka huko kwenda kushindana na wenzetu ili tuweze kuona sasa huku ndani tumemaliza, sasa tunakwenda nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesema suala la leseni. Leo ndani ya Taifa letu tuna leseni; nikiwa nauza mandazi, natakiwa niwe na leseni, nina *guest house,* niwe na leseni, nina magari kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema, lazima niwe na leseni ya magari, sijui nauza duka, lazima niwe na leseni ya duka. Hivi vitu wakati mwingine hebu kama Taifa tujitathmini. Kuna faida gani ya mfanyabiashara mmoja kuwa na leseni saba? Kuna faida gani ya mfanyabiashara Kunti kuwa na leseni saba za biashara? Hivi ni kwa nini kama nchi tusione kuna sababu sasa ya kutoka huko? Kama ni *issue* ya mapato ya Halmashauri, Serikali itengeneze mfumo kwamba mfanyabiashara awe na leseni moja, na Halmashauri itapata mapato yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali, tutakapoingia kwenye hili Azimio, tunapojiunga ni lazima tutoke

sasa kwenye ule mfumo wa kuwa na leseni saba, tutengeneze mfumo wa kuwa na leseni moja ili pia hata hao wenzetu wanaokuja wakute tumeshajipanga kama nchi, tuko *serious* na tunajua nini tunachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili Azimio watakaokwenda kuwajibika ni wafanyabiashara ama ni sekta binafsi na siyo Serikali. Kwa hiyo, ni lazima tutengeneze mazingira rafiki ya kuwa karibu na sekta binafsi na kuwatengenezea mazingira rafiki yatakayoweza kufanya kazi ama kufanya biashara zao bila usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu hapa kuna Wizara mbalimbali ambazo kila Waziri anasimamia sera yake kwenye Wizara yake. Nafahamu Mheshimiwa Waziri ni mratibu kwenye suala la biashara. Sasa kama nchi, ni lazima Serikali muanze iwe na lugha moja. Bila ya kuwa na lugha moja, leo Waziri wa Nishati anasimama na ya kwake, Waziri wa Kilimo anasimama na ya kwake, Waziri wa Fedha akija hapa ana ya kwake, Waziri wa Habari ana ya kwake, Waziri wa Biashara nawe unakuja na *story* zako, hatutaeleweka kama Taifa na itifaki hii haitaleta tija kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ifike wakati pia kama Serikali, kama nchi, ni lazima muanze kuongea lugha moja. Atakachokisema Waziri wa Viwanda akiseme Waziri wa Fedha; atakachokisema Waziri wa Fedha vivyo hivyo Waziri wa Nishati, Serikali tuweze kuwa na lugha moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye itifaki hii pia ni lazima tuandae rasilimali watu wenye ujuzi kwenda kushindana na hawa wenzetu. Tusipoandaa rasilimali watu yenye ujuzi, suala la uwepo wa ongezeko la ajira kwenye nchi yetu itakuwa ni ndoto za Abunuasi. Ajira zitachukuliwa na mataifa ya wenzetu na sisi tutabaki kuendelea kulalamika. Kwa nini? Ni kwa sababu kama Taifa hatukuchukua hatua kuwaandaa watu wetu. Kwa hiyo, ni lazima tuandae rasilimali watu ambao wana ujuzi ili tuende tukashindane na hizo fursa za ajira ikiwezekana tuzibebe nyingi

zaidi kwenye Taifa letu tuweze kupunguza hilo wimbi la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ubora wa huduma. Lazima huduma zetu ziwe na ubora, zikidhi viwango vya mataifa hayo mengine. Tusipokidhi ubora wa huduma zetu pia itakuwa ni changamoto, tutabakia kupokea huduma za watu kutoka kwenye hayo mataifa na sisi tutakuwa na shimo la taka la kujaza matakataka humu ndani ya nchi. Kwa hiyo, lazima tujipange kuwa na huduma ya ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu mfano mdogo sana ambao ulinipata jana. Jana kulikuwa na shida ya umeme, ulikatika na baadaye umeme uliporudi, kukawa na maeneo umeme upo na maeneo mengine umeme haupo. Mimi nina namba mbili za *emergency* za *TANESCO,* nikapiga namba ya kwanza; cha kwanza cha kusikitisha, yaani ile namba ya simu ukipiga, kabla hujahudumiwa, tayari hela imeshaanza kutumika. Kabla hujahudumiwa, wameshachukua hela, halafu hiyo ni namba ya huduma ya mteja anayetakiwa kupewa huduma, unamkata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimepiga namba ya kwanza haikupokelewa, namba ya pili haikupokelewa, nikarudia. Namba ya kwanza ikapokelewa. Ilivyopokelewa nikapewa namba ya usajili wa tatizo nililoripoti, nikaambiwa baada ya nusu saa nitapata huduma. Sikupata hiyo huduma. Nikapiga ile namba ya pili, ikapokelewa, nikapewa namba nyingine tena ya huduma. Yaani taasisi hiyo hiyo moja, kwenye mfumo pale hawezi hata kuona kwamba mita namba hii imeshapewa namba ya huduma hii, tatizo lake linashughulikiwa. Nikapewa tena namba nyingine ya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaona ni namna gani ambavyo kama nchi, hata mifumo yake tu yenyewe bado haijawa bora. Haiwezekani kitengo cha huduma kwa wateja, *emergency call* unapiga namba mbili unapewa majibu tofauti na watu tofauti na wako kwenye *system.* Nilifanya makusudi tu kupiga, niliamini angenijibu akaniambia tatizo lako

limeshapokelewa, linafanyiwa kazi, lakini cha ajabu nikapewa namba nyingine tena nikaambiwa subiri nusu saa. Kwa hiyo, tuone changamoto zilizopo kwenye huduma zetu tunazozitoa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna Bwawa la Mwalimu Nyerere lile pale ambapo tutakwenda kuzalisha umeme ambao utahudumia Watanzania, tunatarajia tuwauzie na wengine. Kama changamoto hata za kwenye mfumo ziko hivi, nani atachukua huo umeme wetu? Hayupo. Kwa sababu watachoka, mtakuwa hamwasikilizi, mnawapa maneno, badala ya kuwapa huduma inayostahili. Kwa hiyo, lizingatiwe pia suala zima la ubora wa huduma zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni matangazo. Tunaweza tukawa na hizo fursa nyingi lakini tusipozifanyia matangazo ya uhakika, yenye tija, pia hali kadhalika hakuna atakayeweza kujua sisi kama Taifa la Tanzania tuna vitu gani ambavyo vinaweza vikaingia kwenye soko hilo la ushindani huko kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la amani ndani ya nchi yetu. Yote haya tunayoyafanya ni lazima kama Taifa tuwe na amani ambayo itaweza kutusaidia…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wake na amezungumza hapa jambo la msingi sana. Changamoto ambazo zimekuwa

zikijitokeza kwenye sekta mbalimbali katika kutoa kuhuduma, biashara hizi za huduma na ametoa mifano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimpe taarifa kwamba kwa kuzingatia maelekezo ya Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Serikali yetu kwa kuzingatia usikivu wa Serikali yetu. Bunge lilitushauri kuanzisha sasa kitengo ama idara maalum ya *monitoring and evaluation* ili kadhia zote zinazojitokeza, ikiwemo kama hii, changamoto za kimfumo katika utoaji wa huduma fungamanishi Serikali iwe na majibu ya jumla na hasa kupitia kwenye mamlaka zetu na hasa mamlaka ya Serikali mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubaliana naye na naomba tu nimpe taarifa kwamba jambo hili tumeshaanza kulifanyia kazi, idara imeshaanzishwa, uratibu unafanyika na huko tunakoingia kwenye *protocol* ya *SADC* haya ni mambo ambayo tulishayaona na tumeshajipanga ili iwe ni sehemu ya utatuzi wa changamoto tunazozipata. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kunti unaipokea taarifa hiyo, uendelee na mchango wako?

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahisi Mheshimiwa Waziri hajanielewa.

Pili, kazi yangu mimi Mbunge na wajibu wangu ni kusema yale tunayoyaona na tunayokutana nayo na tunayoambiwa na wananchi, na kazi yao kama Serikali ni kusikiliza yale tunayoyasema yanayotoka kwa wananchi. Sasa suala la tatu, mkiamua kuyafanyia kazi ni juu yenu, mkiamua kuyapuuza ni hiari yenu. Kwa hiyo, mimi kama Kunti, Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nimetimiza wajibu na jukumu langu ndani ya Taifa langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee. Amani ndani ya Taifa letu. Hii amani tuliyonayo ni muhimu sana katika Taifa letu, na amani inakuwepo tu kama watu watatendewa haki ndani ya Taifa. Haki hiyo ya kwanza ni ya kusikilizwa ambayo ndiyo hii

mnayoifanya; Serikali tusikilizeni. Nikisema hapa, mimi sisemi ya familia yangu, ninasema ya Watanzania huko nje kwa sababu wamekosa fursa ya kuja kuingia ndani humu na kuyasema haya. Kwa hiyo, haki ya kwanza, Watanzania tunahitaji kusikilizwa yale tunayoyasema ili ninyi muweze kuyachakata na kuona ni namna gani mnakwenda kuyafanyia kazi kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipoamua kuwa wasikivu, tukawa na yale maneno ya kusema Serikali sikivu ya mdomoni kwenye moyo haipo, hatutalisaidia Taifa. Kwa sababu hata wawekezaji tunaowategemea, wakiona Serikali yetu inasema bila kutekeleza kwa vitendo, bado watakuwa na hofu na sintofahamu kwamba nikienda pale nitaenda kufanya nini? Kwa sababu Taifa lao lenyewe halina uhakika, watu wao wana vinyongo ndani ya nafsi. Kwa hiyo, naomba amani na suala zima la kusikilizwa lilindwe na lifanywe kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, nakushukuru kwa muda, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, na Mheshimiwa Naibu Waziri ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia suala lililopo mbele yetu, Azimio la Kuridhia Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo niongee mambo mawili makubwa ambayo huwa tunayapata baada ya kupitisha maazimio katika Bunge lako Tukufu. Awali ya yote, nipongeze mtazamo wa Wizara kwa ujumla kwa sababu dunia inapokwenda sasa hivi, sisi hatuwezi kukaa kama kisiwa. Dunia imeshakuwa *globalized,* mambo yanafanyika kwa pamoja. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwamba inawezekana hata kuridhia Azimio hili tumechelewa. Kwa kuwa sasa tumeamua kuridhia, nitakuwa na ushauri wangu katika mambo mawili kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni *timing* au kwenda na muda. Jambo la pili ni *mindset,* jinsi ya kuandaa akili za Watanzania ili kwenda sawa na mipango ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na *timing,* kila kitu lazima kiwe na muda maalum na ili ufikie malengo unayopanga, lazima ujipangie muda. Kamati imeeleza vizuri sana na imetoa ushauri mzuri sana kwamba tunakwenda kuridhia itifaki hii, cha msingi, ni lazima Serikali iangalie sera zetu, kanuni zetu na sheria zetu ziendane na wakati. Maana tunaweza tukaridhia hili, bado sheria zetu zikachelewa kurekebishwa, na kanuni zetu zikachelewa, bado na sera zetu zikawa ni zile zile, haitakuwa na maana ya sisi kuridhia haya. Kwa hiyo, tunaomba haya mambo tunapoyapitisha, yaendane na kasi na muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwetu Iringa kuna usemi tunasema hivi: "Ng'ombe anayewahi kufika mtoni, ndiye anayekunywa maji masafi." Kwenye biashara kuna watu wanaoitwa *innovators.* Wale watu ambao ni *innovators* mara nyingi hawafilisiki na ndio ambao huwa wanaendelea, wanarithisha utajiri kizazi na kizazi. Wale ambao wanajifunza kwa kuangalia matokeo, mara nyingi ndio wale ambao wanafilisika kila wakati. Mtu ambaye anabuni kitu akakianzisha mwenyewe, mwingine anasubiri mwenzie abuni, aangalie kama atanufaika, yule ndiye ambaye sasa anakuja kufilisikafilisika na biashara zake haziendi vizuri; lakini mtu yeyote anayeangalia mapema akawahi ile fursa mapema, ndiye anayeweza kufaidi na kunufaika na hiyo fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaridhia Azimio hili kwa nia ya kwamba sasa tunaenda kuboresha utalii wetu, tunaenda kutanua mipaka yetu ya kunufaika kibiashara kwenye nchi ambazo zinaridhia Azimio hili, lakini wenzetu watanufaika, watafaidi kwenye nchi yetu, na sisi watu wetu wakawa bado wana-*lag behind* au bado hatujawaandaa katika ile *attitude,* ndiyo unakuja sasa kwenye *aspect* namba mbili ya *mindset.* Ni namna gani tunawaandaa watanzania kwenye haya maazimio mazuri ambayo Bunge linayapitisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, akili za Watanzania huwa zinashibishwa vipi maarifa, wakaelewa nia dhabiti ya Serikali inayokuwemo ndani ya haya maazimio? Kama tunapitisha hapa maazimio na Watanzania akili zao hazijaelewa vizuri, bado wanaona tunapoteza muda, lakini huwa yanageuka yanakuwa fimbo. Tunapitisha kwa nia njema kwa kuangalia ustawi wa Watanzania, kwa kuangalia kukua kwa uchumi kwa Watanzania, kwa kuangalia tunavyoongeza fursa za ajira, kwa kuangalia tunavyobadilisha maendeleo ya Watanzania, lakini kwa kuwa *mindset* zao ambazo zinakuja kuleta *attitudes* zao hazikusetiwa vizuri, yanatugeuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitisha maazimio, lakini watu hawajui. Mheshimiwa Waziri lazima tukubali kwamba katika bajeti zetu tunatumia gharama kuwaelimisha watu. Mwalimu alishasema, kama wewe unaona kwamba elimu ni gharama, basi jaribu upumbavu au jaribu ujinga. Kama tunafikiri kwamba tutapitisha maazimio halafu Watanzania hawayaelewi yakaenda yalivyo, hebu tujaribu sasa kuyapitisha maazimio, watu hawayaelewi, halafu uone yakifika kwenye jamii jinsi yanavyoturudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatakiwa kuwekeza nguvu kubwa kwenye kuhakikisha kwamba watanzania wanaelewa nini hasa nia nzuri na dhabiti ya Serikali kwa kuwapa elimu waelewe. Usipom-*set* mtu vizuri kwenye akili aka-*download* uongo akauweka kwenye moyo wake, kuja kuutoa huo uongo aliouweka moyoni ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali, kwenye maazimio kama haya yasiishie tu hapa, lazima kuwe na *program* maalum ya kuhakikisha Watanzania wanaelimishwa, wanawekwa sawasawa, waelewe nia thabiti ya Serikali yao, kwamba nia ya Azimio hili ni kutanua mipaka yetu hata ya ajira. Hatuwezi tukakaa humu ndani ya Tanzania…

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** … na Watanzania milioni 61 tukafikiri kwamba tunaweza kuajiri wote humu tukapata fursa, wakati kuna fursa ya ajira sehemu ya watu milioni 360…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge.

**TAARIFA**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kumpa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Msambatavangu kuwa katika hilo analolisema, ni jambo jema sana na Umoja wa Mataifa tayari imeshaweka Azimio la kwamba *sharing misinformation can seriously harm those around you.* Nafikiri ni wakati sahihi sasa ili watu waweze kuelewa maazimio yanayotolewa na Serikali kwa usahihi, tuunge mkono jitihada za Umoja wa Mataifa katika kampeni hii ya watu kuto-*share* taarifa zisizokuwa sahihi bila kuwa na uhakika wa taarifa hizo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca, taarifa unaipokea?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili, taarifa ya *Engineer* iliyoenda shule.

Mheshimwia Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba taarifa ni nguvu. Azimio hili limeongelea, na sifa kubwa ya nchi yetu ni kuwa na amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie amani na utulivu huwa inaanza kwanza kwenye choko choko za kupotosha taarifa. Tutachokonoa Mhimili wetu wa amani na kukorofishana humu ndani na tukapigana na tukaonekana hatuko sawa sawa baadaye tunakuja kuambizana kumbe kuna muongo mmoja alianzisha tu taarifa akaipeleka yeye isivyo wakati wenye taarifa sahihi hawakuzifikisha wakati sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe maazimio haya yamilikiwe na Serikali kama mnavyotumilikisha Wabunge na Watanzania

wayamiliki haya ni mambo ya nchi yetu, wawe wanaelewa tuna desturi moja. Isiwe rahisi mtu anakuja tu kutuambia tumeuzwa, watu wengine *pressure* zinapanda mmeuzwa, mmeuzwa, mmeuzwa watu wanafikili. Mtu mwingine anaweza akatoka hapa na hili hili azimio akaenda kusema mmekodishwa, mmekodishwa *SADC* watu wakaona tumekodishwa au tumepangishwa. Kumbe nia siyo hiyo nia ni thabiti watu wapewe elimu tutumie fedha kutoa elimu kwa Watanzania wawe wanaelewa mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utali ni *package*, Watanzania waelewe utalini *package*, mtalii anataka kutoka Afrika Kusini mpaka Cairo atumie ile nini wanasema *Cape to Cairo* apite nchi zote ndani ya Afrika akafike Cairo atoke Kusini mpaka kule. Sasa sisi tukikaa tumejifungua hapa hatujaridhia azimio hili tumetanua utalii wetu kupitia *royal tour* watu watatoka Marekani watakuja Tanzania watataka kwenda Congo tayari kuna vifigisu figisu sisi hatujafungua mipaka na kushirikiana na wenzetu wa Congo utalii hautokua? *mindset* za Watanzania hapo wengine tayari ukishaambiwa tu nchi nyingine kama Congo unajua ni vita tu, ukumbuki kumbe na akina Awilo Longomba nao watatoka huko huko kama kuna vita tu hakuna mambo mengine ya starehe kwanini wanaweza kupata muda wakajifunza na muziki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ni ku-*unset mind* zao wajue kwamba kuna fursa kwenye nchi zingine; lazima Watanzania wapate maarifa haya. Ndugu zangu tusipo wekeza kwenye *mind set* na *altitude* tunapitwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda nchi kama Nigeria wanakwambia moja ya sehemu ambapo wameajiri watu wengi ni kwenye utume ni *missionary* namna ambavyo wameshirikiana na Taasisi za kidini halafu wamezifundisha zile Taasisi za kidini wamezi-*empower* kwa kutengeneza kanuni na sera nzuri wamewaruhusu dini waende nje ya mipaka ya nchi yao. Kwa hiyo, wameweza kufungua huko mamisikiti, wameweza kufungua huko makanisa kwa watu wengine wamekwenda kuajiriwa hata nje ya Nigeria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunajipanga vipi kuhakikisha kwamba tunashirikiana na wenzetu, siyo tu sisi Watanzania, Taasisi za dini kuona kwamba tunawaita Viongozi wa dini tukawaambia kuna fursa hizi tunaomba mnaposimama mkitoa maelekezo yenu, mkitoa na nyaraka nyingine toeni na fursa hizi hapa ili Watanzania wajue kuna fursa sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hayo hatutayafanya tutabaki kulaumiana na tutaonekana sisi tunaandika vizuri sana, tunamipango mingi sana, tunamaazimio mengi tunapitisha lakini hayana tija kwa Watanzania…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca ahsante sana, malizia sentesi ya mwisho.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri, narudia tena lazima tuhakikishe tunawekeza kwenye fahamu. Watu wetu wajue na wewe ndiyo Waziri wa Viwanda na Biashara, watu wetu wajue ni kitu gani hasa kiko ndani ya hili azimio?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Isack Mtinga atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Mtoa hoja ajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia itifaki hii ya huduma za kibiashara ya nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza sana Wabunge wenzetu ambao wameendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais ya kuwapa kazi ya kumsaidia katika kuiongoza na kuiendesha nchi yake lakini pia niwape pongezi wale ambao wanaingia kwa mara ya kwanza na hususani Mwenyekiti wetu wa Kamati yetu Mheshimiwa Kihenzile Mwenyekiti wetu hodari sana kwakupata nafasi naamini yale ambayo alikuwa anayafanya

mazuri sana kwenye Kamati yetu sasa anaenda kuyaonyesha kwenye Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niendelee kumpongeza sana Rais wangu kwa jinsi ambavyo anaendelea kuupiga mwingi na nchi yetu inaendelea kunufaika sana na mambo mengi ambayo Rais wetu anayafuatilia. Jimbo langu leo linaogelea mambo mengi sana ya kimaendeleo kwa sababu ya kazi nzuri anayoipiga Rais wetu. Naamini hata hao wachache ambao wamehamishwa hamishwa wataendelea kuyafanya hayo mambo ya kumsaidia Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono kwamba itifaki hii niombe Bunge liipitishe pamoja na kuchelewa kwa muda mrefu sana. Ni kweli miaka mingi imepita takribani kumi na moja tangu isainiwe mtu yeyote anaweza akawa na hofu kidogo kwanini imechelewa? lakini waswahili wanasema chelewa ufike. Tumechelewa lakini sasa tunafika ni jambo la msingi sana kulifanya kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niiombe Serikali sisi kama Bunge tunaridhia sasa lakini wao ndiyo watekelezaji wa hizi itifaki ambazo tunaridhia kwa maana ya kwamba wanakwenda sasa kufanya mikataba mbali mbali *bilateral* kati ya sekta zinazohusika katika utendendaji wa hizi itifakia ambazo tunazipitisha. Kwa hivyo ningewaomba sana Serikali washirikishe sana sekta binafsi kwa karibu sana katika utekelezaji wa hizi itifaki kwasababu wao ndiyo walaji wakubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tukichukulia tu suala la mabenki wafanyabiashara wetu wamekuwa na tabu sana wanapofanyabiashara katika nchi hizi na hasa ukizingia hata sasa kwa mfano tatizo la dola naamini kama nchi hizi zote za *SADC* mabenki yetu yatakua katika nchi hizo, ufanyaji wa biashara utakuwa mwepesi sana. Mtu anaweza akaenda hata nchi nyingine akatumia *local currency* yetu kwa kujua benki yetu iko kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Serikali iziwezeshe benki zetu lakini pia izishirikishe na kuzishauri na kua karibu nao katika kuwahamasisha kuanzisha mabenki katika nchi takribani zote tu za itifaki hii nchi za *SADC* ili hili suala la biashara liwe jepesi sana. Mfanyabiashara akienda nchi ya *SADC* yeyote akaikuta benki yake ya *NMB* au *CRDB* iko kule hata ile imani tu ya ufanyaji wa biashara anakuwanayo lakini pia usaidizi wa karibu wakupata hata anapopata tatizo lolote la kifedha au la kibiashara inakuwa rahisi sana. Kwasababu unahisi kama benki yako ndiyo kama uko kwenye nchi yako tu kwa sababu benki yako unayoijua na unayoiamini iko kule. Lakini vilevile benki yetu itaendelea kufanya biashara katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba sana Serikali iangalie kwa karibu sana jambo hili la kushirikisha mabenki kuhakikisha na kuyawezesha na kuyashauri kwa vyovyote inavyowezena ili kuweza kufungua katika hizi nchi za *SADC* na tuweze kulifaidi vizuri soko hili. Kwa sababu biashara ni fedha, usipokuwa na fedha hamna biashara ambayo utaweza kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuishauri Serikali katika suala la huduma ya afya niwaombe Serikali itimize ndoto ya Rais Jakaya Kikwete ya kuifanya Hospitali ya Benjamini Mkapa kuwa kituo cha kimataifa cha afya pamoja na utafiti. Nahakika kabisa kama tutafanya mambo ambayo yalikusudiwa pale huduma, vifaa na madaktari tunao wengi, madaktari wetu mabingwa wako katika nchi za watu wanatibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninahakika kama tukiwezesha hospitali hii kuwa kituo cha utafiti kikubwa na tiba basi Tanzania ndiyo itakuwa India ya hizi nchi zote za *SADC* na hivyo tutakuwa sasa tunatengeneza utalii, utalii wa kihuduma, utalii wa kimatibabu na hivyo kufanya nchi yetu kupata fedha nyingi za kigeni lakini vilevile kuwa tumeitendea haki itifaki hii katika sekta hii ya huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali hebu hili iliangalie kwa makini tayari kuna kitu kikubwa pale kimeanza ni kiasi cha kuongeza nguvu tu na tutasababisha nchi zote hizi

zikaitegemea nchi yetu. Tiba ni vifaa na madaktari na naamini nchi yetu tuna uwezo mkubwa sana kama tumeweza kujenga mabwawa ya matrilioni, tumeweza kuweka hizi *standard gauge* za matrilioni hatuwezi kushindwa ku-*invest* kwenye afya hapa Benjamini Mkapa na hizi nchi zote zikatutegemea wakaachana na habari ya kwenda India, India yao ikawa hapa Dodoma hapa Tanzania na hivyo kuweza kufanya hii huduma tukatumia vizuri hili soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuangalia Serikali iwezeshe hizi biashara zetu ndogo ndogo kufanyika kwa urahisi Wafanyabiashara wetu wamekuwa wakiteseka sana. Unakuta mtu anaenda kwenye mpaka anabidhaa anaambiwa hii bidhaa hairuhusiwi kuingia huku, kwa mfano kuna nchi zinakataa nyama yetu wakati zipo nchi za jirani zinanua mifugo yetu, zinakwenda zinachinja huko zinapata nyama zinapeleka kwenye hizo nchi ambazo zinakataa, zinasingizia kwamba sisi hatuchanji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaona kuna vihujuma vidogo vidogo ambavyo vinafanyika. Sasa itifaki kama hizi ebu ziwe mwarubaini sasa wa kutibu hizi hujuma ndogo ndogo na Serikali iangalie kabisa kama tuna mahusiano ya kupeana huduma, huduma ziko za aina nyingi sasa huduma siyo tuhujumiane pia. Kwa hiyo, ningependa Serikali iwe makini sana kuhakikisha wafanyabiashara wetu hawateseki na wanafaidi hili soko kubwa kwa kuepukana na hizi hujuma ndogo ndogo ambazo zinafanyika katika biashara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuangalie sheria zetu, sheria zetu zingine zinatushika miguu sisi wenyewe, ningeomba Serikali ebu iangalie kwa makini sheria ambazo zimepitwa na wakati kuna mambo mengine tunajishika miguu wenyewe. Unakuta mtu anataka kupeleka nyama mahala anafika *boarder* au anafika bandarini anambiwa hebu lete cheti cha mionzi, wakati hata hiyo nchi inayopelekewa hizo nyama hata habari ya mionzi hawana, hawajui chochote kuhusu mionzi tunashikana miguu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hebu tuangalie na vitu ambavyo sisi wenyewe vinafanya wafanyabiashara wetu

wanashindwa kufanya biashara na hizi nchi na hivyo kufaidi hili soko kwa kuangalia zile sheria zilizopitwa na wakati turekebishe tufanye mambo ya biashara yawe rahisi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine amelisema mama wa afya ya akili hapa Mheshimiwa Jesca suala la watu kufahamu kupata elimu juu ya hizi itifaki. Niiombe Serikali ni kweli inapoleta suala la itifaki Bungeni ni suala la Kibunge lakini niiombe Serikali iwe na mtindo wa kuwaanda wananchi kwamba sasa tunapeleka itifaki fulani Bungeni, itafaki inayowahusu ninyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu bungeni ndiyo mahali pekee ambako tunaweza kumuita mwananchi, tunaweza kumwita mdau tukaja tukamsikiliza anasema nini kuhusu itifaki tunayotaka kuipitisha. Kwa hiyo, niiombe Serikali ijenge tabia ya kuwahabarisha wananchi, kuwahabarisha wadau kwamba tunapeleka itifaki fulani Bunge inayohusu jambo fulani kule ndiyo mahala ambako mnaweza kwenda kusema. Kwa hiyo, jamii na wadau wanakuwa na habari kwamba kuna itifaki inakwenda bungeni inakwenda kujadiliwa inayotuhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Bunge tunapowaita sasa wadau njooni mseme kuhusu itifaki wanakuwa wanauelewa. Kwa hiyo, tunapata *input* za watumiaji wa hiyo itifaki kwa hiyo, linakuwa ni jambo letu wote tunapolipitisha sasa tunapokuwa hawana habari halafu tunapitisha jambo Bunge tukitangaza sisi Bunge tuna taratibu zetu za kutangaza watu waje. Kwamba njooni msikilize lakini jinsi watanzania wetu tulivyo watu wengine magazeti hawasomi, mitandao hawapitii. Sasa kama Serikali haijawahabarisha vizuri tunapotangaza wadau waje hawawezi kuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano sisi kwenye kamati yetu kuhusu jambo hili tumeaihirisha mara mbili tunataka wadau waje tuwasikilize kwa sababu tu watu wengine hawana *information*. Kwa hiyo, niiombe Serikali katika itifaki mbalimbali mnapotaka kuzileta Bungeni jengeni tabia ya kuwahabarisha wadau, habarisha wananchi kwamba tunapeleka itifaki Bungeni kule ndiyo mahala mnaweza kwenda kutoa *input* zetu ili

tukipitisha linakuwa ni jambo letu na siyo la kutukana Bunge la kulaani Bunge kwa jambo ambalo sisi tumepitisha kwa nia njema, kwa nia ya kuwasaidia wao lakini kwa sababu hawakuwa na habari wanaona kama vile wamesalitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niiombe Serikali ijenge hii tabia ili twende kwa pamoja na wadau wawe wanafaidi hizi itifaki kwa sababu wanakuwa wanazielewa zimepita kwa nini na kwa manufaa gani na hivyo kuzitumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nihitimishe tu kwakusema niliombe Bunge lipitishe hii itifaki kwa sababu ina nia njema lakini twende kwa pamoja na sisi Wabunge katika maeneo yetu tuendelee kuwahabarisha wafanyabiashara na watu wengine wafaidi hizi itifaki ambazo tunazitumia. Kwa sababu nchi yetu ni nchi kubwa yenye kila namna yenye neema na tukiyatumia vizuri itifaki hizi tutaendeleza maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isack Mtinga ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa mtoa hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kutoa machache kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri katika kuridhia itifaki ya biashara ya huduma ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC)* ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutupa uzima na hadi leo kutufikisha hapa kujadili itifaki hii muhimu. Lakini pili nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kuendelea kutumikia nchi yangu katika nafasi ya Naibu Waziri katika Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuruni nanyi pia Viongozi wetu wa Bunge, wewe Mwenyekiti lakini Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote ambao mmeendelea kutuongoza vizuri hapa Bungeni lakini pia ushirikiano mkubwa mnaopata kutoka kwa Wabunge wenzetu katika kujadili masuala mbalimbali ambayo ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki ya biashara ya huduma ni mwongozo unaotoa wajibu wa kila nchi mwananchama wa *SADC* namna ya kushughulikia sekta ya huduma katika nchi yake na hii ni matokeo kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema ni matokeo ya utekelezaji wa itifaki ya biashara ya mwaka 1996 ambayo nayo iliendelea kujadiliwa na utekelezaji wake ukaanza Januari mwaka 2000. Nasema hili kwa sababu kumekuwa na hoja ya kwamba labda sisi tumechelewa sana kuridhia itifaki hii ya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutia saini itifaki hii mwaka 2012 pale Maputo Msumbiji kulikuwa na muda wa majadiliano katika nchi zote ambayo majadiliano hayo yalikamilika mwaka 2019. Kwa hiyo, katika muda huo ilikuwa kila nchi inafanya majadiliano ili kuona namna gani wataweza kunufaika au kushiriki katika itifaki hii ya huduma ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nchi zile kumi na moja ambazo zimeiridhia ni kwamba ni baada ya hapo. Kwa hiyo, ni takribani kuanzia mwaka 2022 takribani mwaka mmoja ndiyo utekelezaji hasa wa hii itifaki umeanza. Kwa hiyo, Watanzania, Waheshimiwa Wabunge hatujachewelewa ni muda muafaka lakini pia kuchelewa huko kwa mwaka mmoja ni muda mzuri ambao na sisi tumejitafakari kuona namna gani tunaweza kushiriki kikamilifu katika itifaki hii ya huduma au biashara za huduma katika Jumuiya ya *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hoja nyingi sana ambazo zimetolewa hapa lakini muhimu kwanza nikuona namna gani tunaboresha sera zetu, sheria na kanuni lakini na mipango mbalimbali ambayo itawezesha sisi kama nchi kuweza kunufaika baada ya kuridhia itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni hoja muhimu na sisi tumeishaanza kufanya hivyo pamoja na mambo mengine sera zetu zinauhushwa na ziko katika ngazi mbalimbali baada ya muda siyo mrefu italetwa hapa Bungeni ili nazo ziweze kupitishwa naamini hiyo itasaidia kuhakikisha tunapoanza baada ya kuridhia, naamini baada ya kuridhia itifaki hii zitatuwezesha kutekeleza vizuri maazimio ambayo yatakuwa yamepitishwa katika azimio hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hoja muhimu sana ambayo sisi kama Serikali kuona namna gani tunawezesha sekta binafsi ili iweze kuwa shindani tuandae baada ya kuridhia itifaki ya biashara za bidhaa *protocol on trade* ya 2000. Sasa wafanyabiashara na wafanyabiashara na bidhaa mbalimbali lakini changamoto imekuwa katika sasa huduma kwamba sasa huduma kwamba mtu anaweza akawa anatoka na bidhaa zake hapa kupeleka Afrika Kusini lakini sasa hauwezi kusafirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo tunayofanya sasa huduma hizi zilizopo ni baina ya nchi na nchi *bilateral* kama ni benki kati ya Tanzania na Burundi au *DRC* mfano hiyo lakini hizi ni *bilateral agreement* kati ya nchi na nchi au makampuni ama makampuni katika kufanyia biashara. Sasa tunataka tuseme katika Jumuiya tuweze kufanya makubaliano namna ya kushiriki katika huduma za biashara. Kwa hiyo, Serikali tunaona ni muhimu sana ndiyo maana nimeleta hapa turidhie ili tuweze kuwahusisha wafanyabiashara wetu waweze kufanya biashara zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi haja kubwa, hoja kubwa ambayo imeelezwa ni namna ambavyo sisi kama nchi kama Serikali tunaendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ili kuweza kushiriki fursa zinazotokana na Jumuiya zetu zilizopo ikiwemo hii ya *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunaendelea kufanya hivyo na tunaendelea kutoa elimu kwa wadau wote ikiwemo wafanyabiashara, sekta binafsi lakini pia kwa wananchi

kwa ujumla ili wajue nini tunafanya kama Serikali ili kuhakikisha tunainua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuweze kuridhia itifaki hii ambayo ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge sisi siyo kisiwa kwa hiyo hatuwezi kujetenga kusema tutashindwa, tutakaa peke yetu wakati wenzetu wanakwenda katika kuridhia itifaki hii na tayari nchi kumi na moja zisharidhia. Kwa hiyo, ni sisi ni muda muafaka baada ya kutathimini na kutafakari kwa kina tunaamini sasa ni muda muafaka kuridhia tuweze kuendelea na sisi kufaidika na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, ahsante sana, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana. Sasa namwita mtoa hoja aje ahitimishe hoja yake. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru tena Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ametuwezesha kujadiliana kwa upendo wa hali ya juu lakini na wivu wa maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru sana wajumbe wa Kamati yetu ya Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kazi kubwa waliyoifanya wakati tunajadiliana jambo hili kwenye kamati, tuliifanya kazi hii kwa uzalendo wa hali ya juu na Kamati yetu wametushauri tukiwa ndani ya kamati na tumechukua ushauri wao na tutaendelea kuufanyia kazi kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu imesema hapa ikatoa maoni na ushauri kwa Serikali wakati wakiwasilisha taarifa yetu hapa ili ilipowasilishwa na Makamu Mwenyekiti wetu mdogo wangu Mheshimiwa Mariam Ditopile. Niwashukuru sana na

nikushukuru mno kwa usomaji mzuri na nia uliyoitanganza. Sisi kama Wizara tumekuelewa, na naamini na wajumbe wote wa Kamati tumekuelewa, basi tunakwenda kutenda jambao nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Kihenzile kwa kutuongoza vyema kwenye Kamati yetu, tangu ilipokuwa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, na hata ilipobadilioshwa na kuwa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo na Uvuvi aliifanya kazi yake kwa uzalendo wa hali ya juu na kwa weledi wa hali ya juu, na hatimaye Mheshimiwa Rais ameweza kumteua na kuwa Naibu Waziri, nampongeza sana. Sisi kama Wizara tunatambua kazi yake njema aliyoifanya kwetu kwa jinsi aliyotushauri. Kama Wizara mawazo yake tutaendelea kuyafanyia kazi pamoja na wajumbe wote wa Kamati yetu. Hakika sisi kama Wizara tunawashukuru sana na tunatambua mchango wenu mwema wa utendaji wa Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru wewe kwa jinsi ulivyoliongoza Bunge letu tukufu siku hii ya leo na siku zote ambazo umekuwa ukituongoza kwenye majadiliano ndani ya Bunge letu hili. Nikushukuru na nikupongeze sana. Tumeyapokea yote yaliyosemwa na Waheshimiwa Wabunge, tumepokea hoja, ushauri pamoja na maelekezo kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge nane waliochangia jambo letu hili ambalo tumeliweka mezani. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuweza kutushauri sisi kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati nawasilisha hoja hii pale mwanzoni, kwamba tayari Serikali yetu ilikuwa inaendelea kushiriki kwenye majadiliano, kwenye utekelezaji wa itifaki hii. Tulikuwa tunashiriki kwa sababu sisi ni wajumbe kwenye Jumuiya yetu ya Maenedeleo Kusini mwa Afrika, lakini tulikuwa hatuna uwezo wa kwenda kutekeleza kile ambacho kilikuwa kinajadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo leo hii Waheshimiwa Wabunge tumelileta mbele yenu, tunawaomba sana muweze kuridhia. Na niwashukuru Wabunge wote nane mliochangia,

mmekubali kuridhia itifaki hii ili kama Taifa sasa twende kunufaika nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya awali naomba nimpongeze sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa utayari wake wa kuona Taifa letu linashiriki kule duniani kupitia diplomasia ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kushirirki vizuri kule duniani kama na majirani zako bado hamjajiimarisha ushirikiano hasa ushirikiano huu wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu alituelekeza na ametoa maelekezo kwa itifaki zetu zote zinazohusu biashara kwenye ukanda wetu, zote ziweze kufanyiwa kazi na tuziridhie. Ni kwa sababu ya utayari wake, wa kuona Watanzania wananufaika na uwepo wa Taifa letu na uwepo wa *benefits* zote tulizonzo ndani ya Taifa letu, *comparative advantage* tuliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema na amekuwa akisema siku zote, tusiendelee kuongelea *comparative advantages* tulizonazo kama Taifa tu na badala yake lazima tuzitumie hizo sasa kunufaisha Taifa letu. Na moja ya utekelezaji wake huu ni kuletwa kwa Itifaki hii leo ya Biashara ya huduma, ili Watanzania washiriki kwa pamoja kunufaika na uwepo wa Taifa letu kijiografia hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, amejibu baadhi ya hoja mabazo Waheshimiwa Wabunge wamezisema, na mimi wala siwezi kuzisema zote. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba hoja zote mlizozitoa zinatuwezesha sisi tunapoingia kwenye majadiliano kule kwenye utekelezaji wa Itifaki hii kwenye Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, tuweze kupeleka hoja za wananchi kupitia nyinyi Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo sina sababu ya kuzijibu zote hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri wangu amesema, kwa hiyo mimi nawashukuru sana mmetupa nguvu mmetupa hoja ya Kwenda kuendeleea kuzisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizisemee mbili tu. Hoja ya kwanza niliyoulizwa ni kwamba, kwa nini tumechukua zaidi ya miaka kumi na tatu hadi leo ndio tunaleta Itifaki hii ndani ya Bunge letu tukufu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge nilianza kulijibu jambo hili tukiwa tunajadiliana hapa. Moja ya sababu ambayo tumechukua muda huu mrefu ilikuwa ni kuwaandaa Watanzania ili tunapoingia waweze kunufaika kwa asilimia kubwa na kuingia kwetu kwenye utekelezaji wa Itifaki hii. Serikali yetu baada ya Mheshimiwa Rais wetu kusaini mwaka 2012 tulitafuta Mshauri Mwelekezi ambaye ni Mtanzania, akazunguka kwenye sekta zote akakaa na wafanyabiashara wetu na hata sekta hizi ambazo tumeweza sasa kuingia tumeona sekta za mwanzo sita ilikuwa zimetoka kwa wadau wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Watanzania ambayo ni sekta binafsi imeshirikishwa kwa asilimia 100. Kwa hiyo hii ilikuwa sababu ya kwanza kwa nini tangu mwaka 2012 hatujaleta itifakii hii ndani ya Bunge letu tukufu, tulikuwa tunawaandaa Watanzania ili waweze kunufaika na itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili lilosababisha tuchukue kipindi chote hiki ni kuandaa miundombinu wezeshi ya kwenda kunufaika na itifaki hii ya Azimio la Biashara ya Huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeandaa Taifa letu miundombinu ya barabara. Taifa letu sasa linaunganishwa na nchi zote tulizopakana nazo, kwa hiyo hii ilikuwa ni mojawapo tuhakikishe tumeungana na mataifa yote kupitia barabara zetu, tumekamilisha. Sasa tuna zaidi ya magari 36,000 yanayopita *on transit* kupitia barabara zetu ambayo ni moja ya miundombinu muhimu ya kuhakikisha huduma zinafika kwenye nchi nyingine. Kwa hiyo ya kwanza ilikuwa ni maandalizi haya ya miundombinu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge mmeongelea kuhusu uwekezaji kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere kuhusu upatikanaji wa nishati ya umeme. Tunaridhia

tukiwa sasa tuko tayari; asilimia 95 ya bwawa letu limekamilika tunaenda kuwa na umeme wa ziada tunaziambia nchi za jirani zetu, nchi zetu tulizonazo kwenye Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, tuko tayari sasa kuwafikishia huduma ya nishati ya umeme. Hiyo yote ilikuwa ni kuwaandaa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu kuanzia Serikali ya Awamu ya Tatu, Serikali ya Awamu ya Nne, Serikali ya Awamu ya Tano na sasa Serikali ya Awamu ya Sita tumewekeza kwa kiwango kikubwa kwenye Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa. Ni wiki mbili zilizopita Mheshimiwa Rais amezindua mkongo mwingine *To Africa 5G,* zile si za kubaki Tanzania. Tunufaike Watanzania lakini tuwaambie nchi za Kusini mwa Afrika kwamba sasa tuko tayari kuwahudumia kupitia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Miundombinu imewekwa vizuri sasa tunapeleka huduma, tunaridhia leo Watanzania tukiwa sote tuna uwezo wa kuwahudumia kwenye sekta zote tulizo nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge na ndugu zangu Watanzania, kwamba hatujachelewa. Tumesema theluthi mbili ya nchi za Kusini mwa Afrika zilizotakiwa kuridhia ili utekelezaji huu uanze zimefikiwa mwaka 2022, Januari, ni mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi hatuko nyuma kwa hiyo tuko tayari kuingia sasa. Na kama ilivyo kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa akisisitiza, kwamba tunapokwenda kujiunga na kanda hizi za kiuchumi na kibiashara tusiingie kama wasindikizaji. Hili pia ninyi Waheshimiwa Wabunge mmesema, kwamba tuingie kama washindani, na ndilo lengo lililokuwa la Serikali yetu. Mazingira sasa ni mazuri, mazingira yameandaliwa tuendelee kunufaika sasa na uwepo wetu kwenye Jumuiya hii ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie jambo moja la mwisho. Nimshukuru sana Mheshimiwa dada yangu Jenista Mhagama kwa kusema, Serikali tunajiratibu. Na hata leo tunapohitimisha hapa ushauri elekezi niliousema mwanzo

alishaainisha sera, sheria na kanuni ambazo zitaonekana kama vikwazo tunapoelekea kule kufanya biashara hii ya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Ofisi ya Waziri Mkuu walishaanza kuturatibu kupitia kitengo alichokitaja Mheshimiwa Waziri; kwa hiyo tumeanza kuzifanyia kazi hizo kwa uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, Serikali tuko tayari, sisi mmesema kama waratibu wa biashara ndani ya Taifa letu tunafanya kazi kwa ukaribu sana na Ofisi ya Waziri Mkuu. Yote tunayaainisha tunamkabidhi Mheshimiwa Waziri Mkuu, na yeye anakaa na sisi kama Serikali; tunaweza kuyashughulikia moja baada ya jingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo sera, nimetaja moja, Sera ya Biashara ya Mwaka 2003, zipo hatua za mwisho katika kupitishwa na Serikali yetu ili iweze kuchukua yote mliyoyasema Waheshimiwa Wabunge, tupo hatua za mwisho na tunaendelea kuifanya kazi. Niwatoe hofu Serikali yetu imeweka miundombinu wezeshi na mizuri, ufanyaji biashara ndani ya Taifa letu umerahisishwa kwa kiwango kikubwa. Mmesemea *issue* ya leseni Serikali tulishaiona tunaendelea kuifanyia kazi, na kupitia Bunge letu Tukufu tuna imani matamanio ya wafanyabiashara wetu wa ndani ya nchi, yatafikiwa lakini pia wafanyabiashara wetu ambao watatoka nje ya nchi kuja kutuletea teknolojia zilizo kule kwenye nchi zao pia nazo tutaendelea kuzishughulikia hatua baada ya hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema maneno haya naomba sasa kuleta kwenye Bunge lako Tukufu Itifaki hii ya Biashara ya Huduma ya *SADC,* Ili Bunge letu liweze kuridhia kama Sheria yetu na Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 163, Ibara ndogo ya 3(e) inavyotuelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imeungwa mkono. Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa kanuni zetu nitawahoji.

Wanaoafiki Azimio la Bunge kuhusu mapendekezo ya kurudia Itifaki ya Bisahara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ya Mwaka 2012 *(The SADC Protocol on Trade in Services 2012)* waseme ndio. Wasioafiki waseme siyo.

Ahsante sana. Itifaki imeungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa hiyo natangaza rasmi kwamba Itifaki hii imeridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania leo Tarehe 31 Agosti 2023. *(Makofi)*

*(Azimio la Bunge kuhusu mapendekezo ya kuridhia Itifaki ya Bisahara ya Huduma ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ya Mwaka 2012 (The SADC Protocol on Trade in Services 2012) Llipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge mliopata fursa ya kuchangia katika mjadala huu lakini niipongeze Kamati yetu ya Viwanda, Biashara, Kilmo na Mifugo pia kwa maoni mazuri na mpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Timu nzima Serikali nzima kwa Itifaki hii muhimu sana kwa mustakabali mkubwa wa Taifa letu. Waheshimiwa niwatakie Serikali utendaji mwema kama ambavyo Bunge limeshauri.

Tangazo moja kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo anawatangazia wajumbe wote wa kamati kukutana katika Ukumbi wa Msekwa C mara baada ya Shughuli ya Bunge kuhairishwa.

Baada ya kusema haya nahairiosha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 03:00 Asubuhi.

*(Saa 5.52 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 1 Septemba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*